



# SUZA

CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR



[www.suza.ac.tz](http://www.suza.ac.tz)

*Kichocheo cha Mabadiliko ya Jamii*



**Ukimuelimisha mwanamke umeelimisha jamii - Rais Mwinyi**

# Salamu za Makamu Mkuu wa Chuo



**W**apenzi Wanajumuiya na Wadau wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA),

Kwa furaha kubwa na heshima, tunawasilisha toleo jingine la Jarida letu la Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA). Jarida hili situ chanzo cha taarifa bali ni dhihirisho la safari yetu ya kielimu na jitihada zinazochoea maendeleo ya kitaaluma, utafiti, na ushirikiano wetu na jamii.

Ninavutiwa sana na ustahimilivu, ubunifu, na bidii inayodhihirishwa na wanafunzi, wahadhiri, na wafanyakazi wetu wote katika kufanikisha azma ya kujenga SUZA kuwa kitovu cha maarifa na mchango kwa maendeleo ya Zanzibar na nje ya mipaka yetu.

Katika SUZA, tunaendelea kushikilia dhamira yetu ya kujenga mazingira bora ya kitaaluma yanayochochea ubora wa elimu, utafiti wa kisayansi, na tafiti zinazogusa maisha ya watu.

Tumefanikiwa kuzalisha maarifa na kutoa mchango kwa jamii kupitia juhudizetu za pamoja, na mafanikio haya yanadhihirika katika safari yetu ya kujenga mustakabali wa elimu na maendeleo.

Kupitia juhudizetu, tunahakikisha kwamba tunaandaa kizazi cha viongozi na wataalam wenyewe maadili, maarifa, na uelewa wa kutua changamoto zinazokabili dunia yetu ya leo.

Tunapoendelea kupiga hatua mbele, ninawahimiza kila mmoja wenu kutumia fursa yoyote inayopatikana kujifunza, kukuza maarifa, kushirikiana, na kuchochaea mabadiliko chanya ndani na nje ya SUZA.

Kujitolea kwenu, ari yenu ya kujifunza, na ushirikiano wenu na jamii ni muhimu sana katika kuimarisha msingi wa taasisi yetu na kuendeleza dhamira ya elimu kwa

wote.

Tutaendelea kuimarisha urithi wa SUZA na kuhakikisha kwamba tunazalisha maarifa yenyeye tija na mchango mkubwa kwa jamii pana.

Kwa dhati kabisa, ninawashukuru kwa kuwa sehemu muhimu ya safari hii.

Natumaini kwamba taarifa zilizomo ndani ya jarida hili zitakuwa chachu ya motisha, msukumo wa mawazo mapya, na msingi wa juhudizendelevu za kujenga SUZA yenyeye mafanikio makubwa zaidi.

Nawaomba tuendelee kushirikiana, kusonga mbele kwa pamoja, na kuweka juhudizetu katika kujenga mustakabali wenyewe nuru kwa vizazi vijavyo.

Ahsanteni sana,

**Prof. Moh'd Makame Haji**  
Makamu Mkuu wa Chuo  
Chuo Kikuu cha Taifa cha  
Zanzibar



### **Na Mwandishi Wetu, SUZA**

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambaye pia ndiye Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) Dk. Hussein Mwinyi amevutiwa na ongezeko la wahitimu wanawake ambao wanaendelea kuongezeka katika programu mbali mbali zinazotolewa katika Chuo hiki.

Alisema katika mwaka wa masomo 2023/2024 wahitimu 2791 wametunukiwa Shahada mbalimbali ambao sawa ongezeko la asilimia 7.7 ikilinganishwa na idadi ya wahitimu 2101 wa mwaka jana.

“Nimefarijika kuona kwa mara nyengine tena tuna idadi kubwa ya wahitimu wanawake kwa asilimia 61 ikilinganishwa na idadi ya wahitimu wanaume ambao ni asilimia 39”, alisema Dk. Mwinyi.

Alifahamisha kuwa hali hii inaleta faraja ikizingatiwa kauli isemayo ‘ukimuelimisha mwanamke umeielimisha jamii’. Kama ilivyo kauli mbiu ya SUZA ‘kichocheo cha mabadiliko ya jamii’

Aliongeza kuwa ana matumaini wahitimu hao watakuwa sehemu ya kuleta mabadiliko chanya katika jamii.

Ameridhika chuo kinaenda sambamba na mabadiliko

ya mitaala kwa kuanzishwa programu nne za ualimu nazo ni Shahada ya Elimu na Michezo na Sayansi ya Michezo, Shahada ya Elimu Mjumuisho na Mahitaji Maalum, Shahada ya Elimu ya Awali na Shahada ya Lughya.

“Uanzishwaji wa program hizi una tija katika sekta ya elimu na kuiwezesha Serikali kufikia malengo iliyojivekea.”, alisema Dk. Mwinyi.

Mapema Makamo Mkuu wa SUZA, Prof. Moh'd Makame Haji alisema SUZA imetekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa kwa mujibu wa mikakati na mipango ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikiwa ni pamoja na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya 2025, Dira ya Maendeleo 2050.

Alielezea matumaini yake kuwa SUZA itatoa elimu bora inayoendana na mahitaji ya jamii na kwenda sambamba na kauli mbiu ya kuwa SUZA ni Kichocheo cha Mabadiliko.

Aliwapongeza wahitimu wote kwa kukamilisha safari yao ya masomo na kuwakumbusha kuwa isiwe mwisho wa kujipatia elimu bali waendelee kutafuta elimu kwani elimu haina mwisho.

“Leo isiwe mwisho wa safari yenu ya mwisho ya elimu baki ianze”, alisisitiza Prof. Haji alisema.

Naye Mwenyekiti wa SUZA, Bi Hamida Ahmed Mohammed, alimshukuru Dk. Mwinyi kwa kwa jitihada zake za kuimarisha Chuo katika nyanja za tafti, taaluma na huduma.

Aidha, aliwashukuru washiriki wa maendeleo kwa msaada mkubwa wanaoutoa katika kuchangia maendeleo mablimbali ikiwa ni pamoja na elimu.

Katika Mahafali haya, Waziri wa nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Haroun Ali Suleiman alitunukiwa Shahada ya Heshima ya Uzamivu (Doctorem Honoris Causa) kutokana utumishi wake wa muda mrefu uliotukuka katika uimarishaji elimu.

Katika mahafali hayo, wahitimu wa fani ya uugazi na ukunga wa Stashahada na Shahada waliapa kiapo cha uaminifu na uadilifu na waugazi na wakunga hawakuwa miongan waliohitimu pia waliasimamishwa kuapa kiapo hicho.

Mahafali hayo yalihudhuriwa na viongozi mashuhuri, wakiwemo viongozi wa zamani, maafisa wa serikali, na wananchi kutoka Zanzibar na Tanzania, ikionyesha jukumu kubwa la SUZA katika elimu na mabadiliko ya jamii.



## Taasisi za Elimu zifanye tafiti - Mheshimiwa Haroun

### Na Mwandishi Wetu, SUZA

**W**aziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria na Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Haroun Ali Suleiman, ametoa wito kwa Taasisi za Elimu za Zanzibar kufanya tafitinyingi zenyematokeo yatakayoleta mabadiliko kwa maendeleo ya jamii.

Akifungua Kongamano la Kitaaluma la kuelekea kilele cha Maadhimisho ya Siku Elimu bila ya Malipo Zanzibar lililofanyika katika ukumbi wa Chuo cha Utalii Maruhubi tarehe 21 Septemba, 2024 Mwalim Haroun alisema kuwa licha ya umuhimu wa kutekeleza, taasisi hizi zinahitaji kuungwa kwa kupatiwa bajeti maalum.

Aidha, aliongeza jitihada za kuimarisha elimu zimekuwa zikichukuliwa na uongozi awamu zote nane tangu mwaka 1964 hadi leo kuwa tunapaswa kutambua juhudzi za Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

“Tumpongeze Dk. Hussein Ali Mwinyi ametuokoa sana”, alikumbusha.

Aidha, aliongeza kuwa awamu ya nane ya uongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imefanya mageuzi mkubwa ya elimu hasa kwa upande wa kupatikana vifaa vya kisasa, kuongeza bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Elimu na miundombinu mingine. Katika hatua nyengine, Mwalimu Haroun Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi alifahamisha kuwa Mzee Karume alifanya jiithada kubwa ya kupambana ubaguzi wa matabaka baina ya watu wenye uwezo ambao walipata fursa zote za elimu na ajira na wasiokuwa na uwezo na wanaotoka mashamba.

Akielezea usoefu wake katika maisha kabla na baada ya Mapinduzi alisema

kuwa ye ye binafsi ni mwathirika wa ubaguzi huo katika familia wakati huo. Mapema, Prof. Moh'd Makame Haji Alifahamisha kuwa Kongamano hili linaenda sambamba na maadhisho ya miaka 60 ya mapinduzi ambayo ndiyo yaliyoleta mageuzi makubwa ya elimu.

Alifahamisha kuwa wananchi walikosa fursa ya elimu katika ngazi mbali mbali kutohana utawala wa wakati huo, suluhisho lililoletwa na muasiwa Taifa hili, Hayati Abeid Amani A Karume, hali inayoendelea kuimarika katika awamu nane mfululizo za uongozi wa Serikali ya mapinduzi Zanzibar.

“SUZA ni mionganini mwa matunda ya Elimu bila Malipo kufuatia kupitishwa kwa sheria mwaka 1999 na Chuo kuanza rasmi mwaka 2021 kikiwa na Idara mbili (2) za taaluma na wanafunzi 108 ambapo kwa sasa kina skuli tisa (9) na taasisi mbili na sasa kuna wanafunzi 7045 na programu zaidi ya 60’, alisema.

Aidha, aliongeza kuwa SUZA imekuwa mhimiili mkubwa wa kufanya tafiti, kutoa taaluma na kutoa ushauri elekezi Serikalini, kutoa suluhisho kwa jamii kjuu ya changamoto mbali mbali zinazowakabili.

Aliongeza kuwa tangu SUZA ilipoanzishwa imezalisha mwahitimuzaidi ya 18,000 uzamili na uzamivu, watu wa aina hii ni vigumu kufanya kazi na degree na watu wa aina hii kufanyakazi katika kwa hivyo eneo la msingilinaloangaliwanikuzalisha vijana wenye ustadi wa ufundi na ujasiriamali. ” SUZA imefanya mazungumzo na taasisi mbalimbali ambazo ziko tayari kuwapokeawahitimuwetu watakaoweza kufanya kazi nao’, alisema Prof. Haji.

Akimkaribisha mgeni rasmi, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Mhe. Lela

Mohammed Mussa, aliwakumbusha wanakongamano na wananchi kwa jumla kuyaenzi Mapinduzi kwani kwani yamewakomboa wanyonge.

Alieleza kuwa jamii inapaswa kutambua kuwa elimu ni chachu ya mabadiliko na maendeleo ya nchi. Naye Mhe. Balozi Mohammed Hamza ambaye ni Mwenyekiti wa Kongamano hilo, aliyahimiza wananchi wa Zanzibar kuenzi na kutunza tunu ya Elimu Bila Malipo kwani ndiyo iliyowakomboa wananchi wanyonge wa visiwa vya Unguja na Pemba.

Akifunga Kongamano hilo, alisitisiza kuwa elimu inayotolewa itosheleze mahitaji ya sasa na yajayo sambamba na kupitiwa sera, mipango, mikakati na uongozi wa Wizara ya Elimu kwani mabadiliko ya dunia yanakwenda kwa haraka mnio.

Muwasilishaji mada, Dk. Bakari Ali Silima kutoka Chuo cha Mafunzo ya Amali Zanzibar alisema maendeleo kwenye fani ya mafunzo ya amali yamekuwa kutoka fani nne lakini hivi sasa kuna fani 22 zinazofundishwa Unguja na Pemba, huku kukiwa na vyuo 57 vikiwemo 16 ya Serikali na 41 ni vya taasisi za binafsi.

Watalamu wengine waliowasilisha mada ni pamoja na Mhe. Balozi Amina Saluma Ali Elimu, Uchumi na Fedha, Dk. Cosmas Mnyanyi Elimu Mjumuisho, Bw. Abdullah Mzee Abdullah Elimu Bila Malipo na Bw. Amour Mtumwa Ali Elimu na Fursa za Utalii.

Kongamano hilo lilloandaliwa na SUZA limewashirikisha watu mbalimbali wakiwemo wasomi, wanataluma katika fani mbali mbali, wakurugenzi, wanafunzi kutoka Vyuo za Zanzibar na skuli mbalimbali za SUZA.



## SUZA, IUCN, CPO wajadili kushirikiana kitaaluma

### Na Mwandishi Wetu, SUZA

**C**huo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kimekutana na ujumbe kutoka Shirikisho la Kimataifa la Hifadhi ya Maumbile na Foundation OCP kujadili namna wanavyoweza kushirikiana katika maeneo yanayofanana ambayo wanayaafanya kazi.

Taasisi hizo zilikutana tarehe 14 Novemba, 2024 katika Kampasi Kuu ya SUZA huko Tunguu mkoaa wa Kusini Unguja ambapo kwa hatua ya awali wamekubaliana kuandaa mazingira ya kuwa na taratibu za ushirikiano huo.

Katika mazungumzo hayo, maeneo ambayo yameonekana yataweza kufanyiwa kazi kwa pamoja ni fani ya utafiti, mabadiliko ya tabianchi, Uchumi wa Buluu kilimo, kuwajengea uwezo wafanyakazi na ubadilishanaji wa teknolojia.

Mkurugenzi wa OCP Foundation Hasina Moukhariq kutoka Morocco alisema taasisi yake inashirikiana na taasisi nyengine ambapo kwa Zanzibar ni taasisi inayohusiana na UChumi wa Buluu na Wizara ya Kilimo na Tanzania Bara ni ofisi ya Waziri Mkuu na WIzara ya Nishati.

Naye Kaimu Mkuu Skuli ya Kilimo, Dk. Burhan Said Ahmed alisema amefurahia kuupokea ujumbe huo ambaa umeonesha nia yadhati kushirikiana katika maeneo mengi ya kitaaluma.

Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), kwa kushirikiana na Shirikisho la Kimataifa la Hifadhi ya Maumbile (IUCN) na Foundation OCP, walikutana tarehe 14 Novemba 2024 kujadili masuala ya ushirikiano wa kitaaluma. Mazungumzo yao yalifanyika katika makao makuu ya SUZA huko Tunguu, Kusini Unguja.

Walilenga maeneo kama utafiti, mabadiliko ya tabianchi, mazungumzo ya uhifadhi wa aina imbalimbali, uchumi wa buluu, kilimo, kuwajengea uwezo

wafanyakazi, na ubadilishanaji wa teknolojia. Hatua ya awali ilikuwa kuandaa mazingira ya kuweka taratibu za ushirikiano huo.

Mkurugenzi wa OCP Foundation, Hasina Moukhariq, aliezeza kuwa taasisi yake inashirikiana na wadau imbalimbali, ikiwa ni pamoja na taasisi zinazoshughulikia uchumi wa buluu Zanzibar na wizara za kilimo na nishati Tanzania Bara. Kwa upande wake, Kaimu Mkuu wa Skuli ya Kilimo SUZA, Dk. Burhan Said Ahmed, aliezeza kufurahishwa na nia ya dhati ya kushirikiana katika nyanja nyingi za kitaaluma.

Shirikisho la Kimataifa la Hifadhi ya Maumbile (IUCN) ni mamlaka ya kimataifa kuhusu hali ya maumbile ya asili na hatua zinazohitajika ili kuyahifadhi.

Ilianizhwa mwaka 1948, IUCN ni muungano wa wanachama unaojumuisha mashirika ya kiserikali na asasi za kiraia, ikiwa na zaidi ya mashirika 1,400 ya wanachama na karibu wataalamu 17,000 wanaochangia katika dhamira yake ya kuendeleza maendeleo endelevu na kuhifadhi mazingira. IUCN inajishughulisha na utatuaji changamoto za kimazingira duniani na kukuza matumizi endelevu ya rasilimali za asili.

Kwa upande mwingine, Mradi wa Open Compute (OCP) ni jamii ya kushirikiana inayolenga katika kubuni upya teknolojia ya vifaa ili kusaidia kwa ufanisi mahitaji ya kuongezeka kwa miundombinu ya kompyuta.

## SUZA yapata mtaalamu elimu ya michezo

### Na Mwandishi Wetu, SUZA

**C**huo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kimepokea mtaalamu atakayefundisha elimu ya sayansi ya michezo kwa ajili ya kuimarisha sekti hiyo katika Chuo hicho.

Akizungumza na mtaalamu huyo, Yutaka Ide anatokea Hiroshima nchini Japani, mazungumzo yaliyofanyika makao makuu ya SUZA Tunguu mkoaa wa Kusini Unguja, Makamo Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Moh'd Makame Haji alisema amefarajika sana kuona sekti hiyo inaimarika kwa kuwa na wataalamu wa ndani na nje.

"Kutokana na uhusiano mzuri baina ya SUZA na Japan kupitia Shirika la JICA wametupatia mtaalamu wa kujitolea ambaye atatufidisha elimu kwa michezo na sayansi ya michezo kwani hatuna wataalamu wa kutosha", alisema Prof. Haji.

"Karibuni tutajenga viwanja vyenye huduma na vifaa vyote vya michezo tunavyohitaji kama vile kuogelea gym na nyengine", alisema.

Prof. aliahidi kuwa mipango ya kukamilisha taratibu itamazilika

muda mfupi ujao ili aanze kazi ya kufundisha elimu kwa michezo na sayansi ya michezo.

Katika kikao hicho ambacho kilimshirikisha pia mtaalamu wa ndani wa fani ya michezo, Ali Rashid Juma, Prof. Haji alisema kuwa anaamini kuwa kila upande utajifunza zaidi katika masuala ya michezo.

Aliongeza kuwa hivi sasa SUZA inatumia eneo dogo la Skuli ya Elimu kwa sababu hakuna vifaa vya kutosha isipokuwa vifaa vyengine vinatumia kutoka kwenye taasisi nyengine.

Aidha, Prof. alifurahishwa na mtaalamu huyo kuwa anaweza kuzungumza Kiswahili na kumshauri ajiunge na taasisi ya SUZA inayofundisha lugha kikiwemo Kiswahili kwa wageni.

Naye Yutaka alisema anakipenda Kiswahili, anafurahia kujifunza na kwamba anatenga muda kwa ajili ya kujifunza lugha hii kila siku.

Naye mkuu wa Skuli ya Elimu, Dk. Said Khamis ambaye alifuatana na mgeni huyo alisema wana matarajio kuwa malengo yaliyowekwa ya kuimarishwa sekti ya michezo yatapatikana muda mfupi ujao.



## Kamati ya Bajeti yajifunza utekelezaji miradi ya SUZA

### Na Mwandishi Wetu, SUZA

**K**amatii ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar imeambatana na uongozi wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) katika ziara ya kujifunza kuhusu utekelezaji wa Mradi wa Higher Education for Economic Transformation (HEET). Ziara hiyo ilifanyika na tarehe 18 Novemba, 2024 katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) kilichopo Mkoo wa Mbeya baada ya kikao cha kamati hiyo kilichopokea taarifa ya utekelezaji wa mradi wa HEET SUZA kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025.

Ziara hiyo ililenga kujifunza na kubaini mafanikio, changamoto, na hatua zinazochukuliwa katika utekelezaji wa Mradi wa HEET katika chuo hiki cha Mbeya, ili kuhakikisha kuwa mradi huu unatekelezwa kwa ufanisi na unaleta matokeo yaliyotarajiwa. Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi ilipokelewa na uongozi wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia, Mkoo wa Mbeya. Wajumbe walipata fursa ya kutembelea na kujionea miundombinu ya Chuo na kupewa maelezo kuhusu Chuo na utekelezaji wa mradi wa HEET.

Uongozi wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Tanzania ukiongozwa na Makamu Mkoo wa Chuo Prof. Aloys Mvuma uliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa mradi wa HEET, ikiwemo mafanikio yaliyopatikana hadi sasa, changamoto zilizojitekeza, na mikakati iliyopo ya kuzitatu. Taarifa ilijikita zaidi katika maeneo ya ujenzi wa miundombinu, upatikanaji wa vifaa vya kufundishia, na maendeleo ya kitaaluma.

Kabla ya kuwasilishwa taarifa hiyo, Kamati ilitembelea maeneo ya ujenzi yanayofadhiliwa na mradi wa HEET, ikiwa ni pamoja na jengo la taaluma, maabara, madarasa, kituo cha ubunifu na uboreshaji wa ubunifu wa kibashara. Wajumbe walijionea maendeleo ya ujenzi na ubora wa vifaa vilivyonunuliwa kwa ajili ya kuimarishe mazingira ya kujifunza.

Wajumbe wa Kamati walipata fursa ya kuuliza maswali na kutoa maoni yao kuhusu utekelezaji wa mradi wa HEET. Maswali mengi ilijikita katika kuhakikisha uwazi na uwajibikaji katika matumizi ya fedha za mradi, pamoja na mkakati wa kudumu wa kukuza ubora wa elimu inayotolewa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Mheshimiwa

Mwanasha Khamis Juma, ambaye pia ni Mwakilishi wa Jimbo la Dimani, alielea kuridhishwa na hatua zilizochukuliwa katika utekelezaji wa mradi wa HEET. Halik adhalika, alipongeza juhudzi za uongozi na watendaji wa hicho kwa kufanikisha miradi mbalimbali licha ya changamoto zilizopo pia aliipongeza SUZA kwa hatua iliyofikia na kuitaka iendelee kupata uzoefu ili kuongeza kasi zaidi ya utekelezaji. Mwenyekiti alizitaka taasisi zote zinazohusika kushirikiana kwa karibu ili kuhakikisha malengo ya mradi yanafikiwa kwa ufanisi. Aidha, alisitisiza umuhimu wa kuweka mikakati endelevu ya kushughulikia changamoto zinazojitekeza ili kuboresha zaidi utekelezaji wa mradi.

Nae Mkamu Mkoo wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Prof. Moh'd Makame Hajji, alitoa maelezo kuhusu fursa ambazo SUZA inapata kujifunza kutoka kwa watekelezaji wa mradi wa HEET. Alielea kuwa ushiriki wa SUZA katika mradi huu unatoa nafasi muhimu ya kujifunza mbinu bora za utekelezaji wa mradi mikubwa ya elimu, ikiwemo usimamizi wa fedha, ujenzi wa miundombinu, na ufundishaji wa kitaaluma. Vilevile, Pro. Hajji alibainisha kuwa mradi wa HEET una nafasi kubwa katika kuimarishe sekta ya elimu ya juu Zanzibar kwa kuongeza uwezo wa Chuo kuzalisha wahitimu wanaohitajika na soko la ajira.

Kupitia mradi huu, SUZA inaimarisha vifaa na miundombinu ya kufundishia na kujifunzia, na kutoa mafunzo kwa wahadhiiri ili kuboresha ubora wa elimu. Hii inasaidia kuwaandaan wanafunzi kwa mahitaji ya soko la ajira, hivyo kuchangia katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya Zanzibar. Makamu Mkoo alisitisiza kuwa ushirikiano na kujifunza kutoka kwa watekelezaji wa mradi ni muhimu katika kufanikisha malengo haya na kuboresha zaidi sekta ya elimu ya juu.

Kwa upande mwengine, Dkt. Everest Mtiti, Msaidizi Mratibu Mkoo Kitaifa, ambaye pia alimuwalikisha Katibu Mkoo wa Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, alizungumzia umuhimu wa mradi wa HEET kwa taifa la Tanzania. Alisitisiza kuwa mradi huu ni muhimu kwa maendeleo ya sekta ya elimu ya juu nchini Tanzania, kwani unalenga kuimarishe mazingira ya kujifunzia na kufundishia, hivyo kuongeza ubora wa elimu inayotolewa.

Dkt. Mtiti pia alielea umuhimu wa kuwa na ushirikiano katika kutekeleza mradi huu ili

ukamilike kwa ufanisi. Alionya kuwa iwapo taasisi moja itashindwa kutekeleza majukumu yake, mradimzima taathirikana kuingadosari. Hivyo, alisitisiza juu ya umuhimu wa mshikamano na ushirikiano baina ya taasisi zote zinazohusika ili kuhakikisha mafanikio ya mradi wa HEET kwa manufaa ya taifa zima.

Zaira hii pia ilitoa nafasi kwa Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi kutembelea ofisi za Mkoo wa Mkoo wa Mbeya ambapo walikaribishwa na Mkoo wa Wilaya Mhe. Beno Malisa ambaye alisema kuwa ziara hii ni fursa ya kubadilishana uzoefu na kujifunza kutoka kwa kila upande. Mkoo wa Mkoo aliahidi kuendelea kushirikiana na SUZA na taasisi nyiningine za Zanzibar katika juhudzi za kuboresha elimu na maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Katika kutoa shukurani za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mheshimiwa Lela Muhammed Mussa, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, alitoa pongezi kwa serikali zote mbili na kuwapongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dr. Samia Suluhu Hassan pamoja na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kwa jitihada kubwa wanazochukua katika kuiletea maendeleo nchi yetu.

Alielea kuwa mradi huu ni wa kitaifa na unahusisha pande zote mbili za Muungano, na mafanikio yake ni kuboresha sekta ya elimu na kuleta maendeleo. Aidha, aliwataka wasimamizi wa mradi kuwa makini na kuongeza nguvu katika usimamizi na kuhakikisha wale wote walipata fursa za kusoma kupitia mradi huu wanamaliza kwa wakati na wanaruudi kufanya kazi ili lengo la mradi lifanikiwe.

Kwajumla, ziaraya Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia, Mkoo wa Mbeya, ilikuwa na mafanikio makubwa. Kamati iliridhika na maendeleo yaliyofikiwa katika utekelezaji wa Mradi wa HEET, pamoja na juhudzi zinazofanywa na chuo katika kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia.

Kamati inapendekeza kwamba juhudzi zaidi zifanyike kushughulikia changamoto zilizobainishwa ili kuhakikisha kuwa mradi huu unatekelezwa kwa ufanisi na unaleta matokeo yanayotarajiwa. Aidha, imetoo wito kwa pande zote zinazohusika kuendelea kushirikiana na kuwekeza katika elimu ya juu kwa maendeleo endelevu ya Tanzania.



## SUZA yashiriki Maonesho ya Siku ya Chakula Duniani, yaja na ajenda ya uajiri kwa vijana

### Na Mwandishi Wetu, SUZA

**M**AKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar Mhe. Hemed Ali Suleiman ametoa wito kwa vijana kutumia fursa zinazowekwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ili waweze kuzalisha mazao na kukuza ufugaji nchini.

Aliysema hayo katika ufunguzi wa maonesho ya Siku ya Chakula Duniani yaliyofanyika katika Mkoa wa Kusini Pemba huko Chamanangwe ambapo aliyahimiza mabaraza ya vijana kutumiwa kwa tija ili yawe mkombozi wa nchi yao katika kukuza uchumi.

Katika Maonesho hayo ambayo yalishirikisha taasisi mbalimbali za serikali na kibinasi kutoka Tanzania bara na Zanzibar, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar pia kilishiriki kikamilifu ambapo Makamu Mkuu wa SUZA,

Prof. Moh'd Makame Haji alisema Chuo kimeanzisha utaratibu maalum wa kuwapatia elimu wanafunzi itakayowawezesha kujajiri ikiwa ni azma ya kutekeleza mipango ya Serikali ya kupambana na umasikini. Kupitia mikakati mbali mbali iliyojiwekea ya kuleta mabadiliko ya jamii kupitia elimu, Chuo kimekuwa kikiandaa shughuli mbalimbali za kunufaisha jamii na wananchi wake.

Kwa kutumia mbinu hizi, wana SUZA na wanajamii wanapata fursa ya kukaa pamoja na kubadilishana mawazo sambamba na kujifunza mambo mengine ya kijamii katika jamii wanayoismamia utekelezaji wa shughuli za kielimu kwa vitendo.

Prof. Haji alieza kuwa Chuo kinatoa elimu kwa makundi kupitia Skuli ya Kilimo kupitia programu za kuwafikia wakulima waliopo Unguja na Pemba kupitia mradi wa TANRICE kwa kuwapatia elimu na mbinu bora za kilimo cha mpunga na mazao mengine.

Alisema kwa utumiaji wa mbinu hii,

wanajamii wamefaidika na uzalishaji mkubwa wa mazao mbali mbali ya kilimo na biashara lakini wamejenga ukaribu wa kuelezea changamoto za kilimo kwa wataalamu wa SUZA ambao huwafanya ziara za kitaalamu mara kwa mara.

Mapema, Waziri wa Kilimo Umwagiliaji, Maliasali na Mifugo, Mhe. Ali Abdallah Shamata alisema ujumbe wa mwaka huu ni; Haki Kupata Chakula kwa Maisha Bora ya Sasa na Baadae unalenga kuongeza maarifa kwa wakulima, kuimarisha lishe kipato, kupata

tija na kipato kwa uchumi wa Taifa. Alieza kuwa Mpango wa mageuzi wa Sekta ya Kilimo na mipango mbali mbali mikakati ya nchi sambamba na Ilani ya CCM ya 2025 vyote vinalenga kuimarisha sekta hii.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Ndg. Ali Khamis alisema hii ni mara ya kufanyika maonesho katika viwanja vya Chamanagwe ambapo mwaka huu taasisi 130 kutoka Tanzania Bara na Visiwani zimeshiriki kuonesha teknolojia na utaalamu wao katika sekta ya kilimo.

## SUZA yachangia kuanzishwa kituo cha Utafiti JWTZ

### Na Jaku Ali, SUZA

**M**akamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Prof. Moh'd Makame Haji amesema analishukuru Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) kwa kuwashirikisha kuwa sehemu ya kuchangia andiko la kuanzishwa kwa Kituo kikubwa cha Tafiti cha Jeshi hili.

Hayo aliysema katika makao makuu ya SUZA huko Tunguu Mkoa wa Kusini Uguja wakati akizungumza na ujumbe wa maofisa kutoka Jeshi la Wananchi tarehe 17/12/2024, Prof. Haji alisema SUZA ina uzoefu katika kuendesha tafiti kwa kushirikiana na vyuo mbali mbali vya Tanzania na taasisi za kimataifa.

Alifafanua miongoni mwa tafiti zilizowahi kufanya ni kama vile zinazohusiana na ukuaji wa lugha ya Kiswahili, sayansi ya bahari, nanyegine zinazowashirikisha jamii ambazo zinatoa suluhisho la changamoto zinazowakabili wanajamii hao.

“Chuo pia kina vituo vya ubunifu ambavyo vimekuwa vikifanya tafiti na kuwaibua vijana wanaofanya kazi kubwa za kutambuliwa”,

Ujumbe wa maofisa wa jeshi Tanzania umekutana na wanataluma wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kujadili namna ya kuratibu tafiti zinazoendeshwa katika taasisi zao.

Mkutano huo ulifanyika tarehe 18/12/2025 katika Makao Mkuu ya SUZA Tunguu Mkoa wa Kusini Uguja ulijadili kwa kina masuala muhimu yatakayowawezesha wanajeshi wanaotaka kuandika andiko la kuanzishwa Kituo cha Taifa cha Jeshi la Wananchi wa Tanzania.

Akizungumza katika kikao hicho, Kanali Morris Ndeshiuta alisema azma ya kuanzishwa kwa kituo cha tafiti inalenga kuongeza uwekezaji na nguvu ya kijeshi hasa wakati huu ambao taasisi hiyo inatumia teknolojia yakisasa.

Alisema Jeshi la Polisi limefanya mambo mengine ambayo yanahitaji kutunzwa na kuhifadhiwa kwa ajili ya vizazzi vijavyo viweze kuyatambua. “Tunashukuru sana kwa mchango wenu kwani tumepokea mawazo mengi na mazuri zaidi ya tulivyo tarajia”, alisema Kanali Ndeshiuta aliyeongozza ujumbe watu saba kutoka JWTZ.

Aliungeza kuwa wameridishwa na michango na fursa walizopewa za kuwatumbua wataalamu wa SUZA katika kufikia malengo walijojiwekea.

Mkutano huo uliwashirikisha pia wakuu wa taasisi na wataalamu katika fani mbali mbali za zinazohusiana na masuala ya utafiti wa Chuo hiki ambao walichagia namna bora ya kuanzishwa kwa Kituo cha Tafiti cha Jeshi.



## SUZA yashiriki Kongamano la Kiswahili Cuba

### Na Mwandishi Wetu, SUZA

**K**ongamano la Kimataifa la Kiswahili limefanyika katika mji wa Havana, nchini Cuba, tarehe 8 na 9 Novemba, 2024. Kongamano hili limehusisha wataalamu na wadau wa Kiswahili kutoka Tanzania na nje ya Tanzania pamoja na wenyeji wa Cuba. Jopo kutoka Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) likiongozwa na Makamu Mkuu wa Chuo, Profesa Moh'd Makame Haji, limeshiriki katika kongamano hilo.

Kongamano hilo lilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wakiwemo Mawaziri wa Mambo ya Nje na Mawaziri wanaosimamia masuala ya utamaduni na michezo pamoja na mabalozi kutoka Tanzania na Cuba. Kongamano hilo lilitunguliwa rasmi na Mhe. Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo wa Tanzania, Dk. Damas Daniel Ndumbaro, kwa niaba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk.. Samia Suluhu Hassan ambaye amesisitiza maendeleo ya Kiswahili barani na nje ya Afrika. Takriban washiriki 400 kutoka Afrika, Asia, Amerika na Ulaya wamehudhuria.

Mbali na maendeleo ya lugha, kongamano hilo pia limejumuisha uhusiano mwema kati ya Tanzania na Cuba yaliyoanzishwa na waasisi wa mataifa haya mawili, Mwalimu Julius K. Nyerere na Fidel Castro. Tamaduni zaonanamna uhusianowao hayo utakayyochochea maendeleo ya nchi pia yamejadiliwa kwa kina.

Katika sherehe za ufunguzi wa kongamano hilo, vitabu vitatu vilizinduliwa kikiwemo. "Jifunze Kihispania kwa Lugha ya

Kiswahili", kilichoandikwa na wahadhiri Dk. Said Suleiman Khamis na Bi. Shani Suleiman Khalfan na kuchapishwa na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.

Kitabu hiki ni mionganoni mwa kazi mpya za SUZA zinazota maarifa ya usomaji na ufundishaji wa lugha za kigeni na maelezo ya kujifunza Kihispania yametolewa kwa lugha ya Kiswahili. Uzinduzi wa kitabu hiki unaashiria uwezo wa SUZA kusanifu Kiswahili na kukifanya kuwa lugha ya kufundishia.

Katika mkutano huo, mada zaidi 20 ziliwasilishwa katika kongamano hilo, zikiwemo zilizoandaliwa na wataalamu kutoka katika nchi hizo. Kwa upande mwengine, SUZA ilitoa mchango wake kupitia wahadhiri na wanafunzi waliotayarisha makala zilizowasilishwa na kuchangiwa katika mijadala iliyofanyika.

Andiko la "Mikakati Bora ya Ufundishaji na Ufunzaji wa Lugha ya Kiswahili kwa Wageni" lililoandaliwa na Dkt. Maryam Ismail kwa kushirikiana na Profesa Alwiya Omar pia liliwasilishwa. Mada hii ambayo imetoa mchango wa mbinu za kisasa za ufundishaji wa lugha ya Kiswahili kwa wageni.

Mbali na wahadhiri kuwa na mchango mkubwa katika kufanikisha kongamano hilo kwa maandalizi na utoaji wa makala za kitaaluma, Mhe. Riziki Pembe Juma, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, ambaye pia ni mwanafunzi wa Shahada ya Uzamivu ya Kiswahili kutoka Skuli ya Kiswahili na Lugha za Kigeni ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, aliwasilisha makala ya "Mchango

wa Wanawake katika Maendeleo ya Kiswahili Duniani: Mifano Kutoka kwa Samia Suluhu Hassan", akishirikianana Ahmad Y. Sovu.

Wasilisho hilo lilijielekeza kuainishana kujadidili mchango wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia katika kuimarisha lugha ya Kiswahili na kuitangaza ndani na nje ya mipaka ya Afrika. Ilielezwa kuwa Kiswahili ni lugha pekee ya Afrika inayotambulika ulimwenguni kote kama lugha ya kimataifa.

Mbali na yaliyojiri katika kongamano hilo, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kimepata fursa ya kufanya mazungumzo na vyuo vikuu mbali mbali vya Cuba kwa lengo la kuanzisha uhusiano ya kitaaluma yatakayohusisha kubadilishana wataalamu na kuongeza ujuzi wa fani mbali mbali.

Jitihada za SUZA katika kukifanya Chuo kuwa cha kimataifa zimeimariswa kupitia ushiriki wake katika kongamano hili. SUZA imekuwa ikifanya kazi kwa bidii kuongeza kasi ya ushirikiano na taasisi nyingine za kimataifa ili kuimarisha elimu na utafiti. Kongamano hili limetoea fursa muhimukwa SUZA kuonesha uwezo wake wa kitaaluma na kuendeleza ushirikiano na vyuo vikuu vya Cuba na taasisi nyingine duniani.

Kwa kupitia jitihada hizi, SUZA inakusudia kuongeza ubora wa elimu inayotolewa na kujenga nafasi yake kama chuo kikuu cha kimataifa kinachotoa elimu bora na yenye ushindani inayokwenda sambamba na kauli mbiu yake ya Kichocheo cha mabadiliko.



## SUZA yazindua maktaba ya kimtandao

### Na Mwandishi Wetu, SUZA

**M**akamu Mkoo wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) Prof. Moh'd Makame Haji amezindua mfumo mpya wa masomo ya kimtandao 'MyLoft - My Library of Finger Print' ambao utasaidia upatikanaji wa tarifa za kimasomo kwa njia rahisi.

Alisema mfumo huo utachangia kuwawezesha wanafunzi na wafanyakazi kufanya kazi zao hasa ikizingatiwa kuwa kumekuwa na ongezeko la wanafunzi wanaosajiliwa kujinga na SUZA kila mwaka.

Dk. Khamis Salum, akimwakilisha Makamu Mkoo wa Chuo, alisisitiza uwezo mkubwa wa kibunifu wa chombo hiki katika kuboresha juhudzi za kielimu za wanafunzi. Aliwahimiza wanafunzi kutumia rasilimali hii ili kupanua upatikanaji wao wa nyenzo za masomo, kurahisisha masomo yao, na kushiriki kwa ufanisi zaidi katika majukwaa ya kujifunza mtandaoni. Kwa kutumia chombo hiki, wanafunzi wanaweza kuimarisha maarifa yao, kuboresha ujuzi wa kitaaluma, na kuijiandaa kwa mahitaji makubwa ya ushindani wa elimu duniani.

Dk. Salum alisisitiza umuhimu wa teknolojia katika masomo ya kisasa na akawataka wanafunzi wote kutumia kikamilifu fursa zinazotolewa na chombo hiki. Naye Mkurugenzi wa Maktaba SUZA, Bw. Moh'd Khamis Kombo alisema umefika wakati wa kutumia teknolojia ya kukusanya taarifa za kielimu kinyume na miaka 30 iliyopita.

"Tumehangaika sana hadi kufikia hapoa tulipo, hatukuinunua ili iwe pambو tunaamini nyinyi ndio watumiaji wetu", Mkurugenzi aliwaambia wageni walioshiriki uzinduzi huo.

Alisema katika kipindi hicho hakukuu na app ya ksuaidia kupata taarifa na badala yake vitabu kutoka maktaba ndio nyenzo muhimu zilizokuwa zikitumiwa.

"Zamani tulipaswa kuvifuata vitabu maktaba lakini sasa App hii inapatikana mahala popote, iwe nyumbani, sokoni au njiani utajifunza mambo mengi kwa mujibu wa mahitaji yako ya kielimu", alisisitiza Mkurugenzi huyo. Naye Meneja wa Kanda ya Afrika wa RemoteXs, Mtaalamu Sila Too, alisema kabla ya matumizi ya mfumo huo, vitabu vingi havikweza kusomwa seuze kuazimwa.

"Baada ya kuona changamoto hii tukaona nivyematuandae programuhii

inayotumiwa bila internet", alieleza Aidha aliongeza kuwa mfumo huu nimashuhuru katika vyuo vikuu vingi nya Afrika ikiwa ni pamoja na Kenya (133), Uganda (33), Ghana (52) na vyengine ni Zambia na Malawi na Botswana na sasa Tanzania ambayo fursa hii inatumika kwa wingi katika vyuo vikuu kadhaa.

Alisisitiza kuwa mfumo huu unatumia na vyuo kuongeza maudhui yake lakini pia kwa wenye vitabu wanaotaka visomwe mtandaoni pia huduma hii inaweza kuingizwa. Aliwakumbusha wanafunzi na wafanyakazi kuwa teknolojia hii inaliipiwa gharama kubwa na vyuo vinavyoitumia hivyo si busara kuwepo bila ya kutumiwa na wanafunzi na hata wafanyakazi wa SUZA kwa matumizi ya kielimu.

## SUZA yaridhishwa mijadala na BADEA

### Na Mwandishi Wetu, SUZA

**N**ainbu Makamu Mkoo wa Chuo cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Dk. Hashim Hamza Chande, ameelezea jamii ya SUZA imeridhishwa na mijadala iliyoiibiliwa baada ya kuwasilishwa mada zilizohusiana na utekelezaji wa mradi wa upanuzi wa Chuo hiki.

Akifunga mkutano wa siku mbili wa uzinduzi wa mradi huo uliofanyika katika Hoteli ya Golden Tulip Uwanja wa Ndege, Dk. Chande alisema mijadala hiyo imesaidia kuonesha njia itakayowawezesha kuepukana na changamoto wakati wa utekelezaji wa mradi huo utakaoanza rasmi 2025 hadi Disemba 2027.

Aidha, aliahidi ushirikiano wakati wote wa utekezaji ili kuhakikisha mradi huo unatekelezwa kama iliyopangwa. Mratibu wa mradi huo Bi. Salma Kimara amewashuku BADEA kwa mchango mkubwa wa kuiwezesha SUZA kukamilisha mpango

wake wa Upanuzi wa Chuo hiki. Mohammed Salum, Kamishna wa Mpango wa Taifa, amesema ndoto ya kupanua SUZA na hatimaye kufikia utekelezaji wake inakwenda sambamba na Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050, Dira ya Dunia ya Maendeleo Endelevu na Agenda ya Afrika ya kuimarisha sekta ya elimu.

Aidha aliahidi kuwa Kamisheni anayoiongoza iko tayari kutoa ushirikiano wowote unaohitajika kwa lengo la kufikia malengo yaliyowekwa. Katika shughuli hiyo, Makamu Mkoo wa SUZA Prof. Moh'd Makame Haji aliwakabidhi zawadi wageni wawakilishi wa kutoka Benki ya Badea walioshiriki uzinduzi uliofanyika jana.

Moja ya zawadi aliyokabidhi ni kumbukumbu ya Zanzibar Door ambapo alisema anawakabidhi mlango huo (ambao aliufungua) akiwa na maana kuwa mlango uko wazi na kwamba wakati wowote wanakaribishwa Zanzibar.



## Lishe duni inachangia vifo vya mama, watoto

### Na Mwandishi Wetu, SUZA

**M**ke wa Rais wa Zanzibar, Mwanzilishi na Mwenyekiti wa Bodii ya Wadhamini wa Zanzibar Maisha Bora Foundation (ZMBF), Mama Mariam Hussein Mwinyi, ameeleza kuwa ukosefu wa mlo kamili unahatarisha maisha ya wanawake wajawazito na watoto.

Akizungumza katika hafla ya usimamizi wa maarifa na mafunzo kuhusu kuboresha huduma za ujumuishaji wa VVU, Kifua Kikuu (TB) na malaria katika huduma za kliniki za kabla na baada ya kujifungua (ANC na PNC) iliyofanyika katika Hoteli ya Golden Tulip Uwanja wa Ndege wa Zanzibar, tarehe tarehe 8 Oktoba, 2024, Mama Mariam aliongeza kuwa lishe duni ni chanzo kikuu cha viwango vya juu vya vifo vya akina mama na watoto Zanzibar.

Alisifujuhudiza Liverpool School of Tropical Medicine (LSTM), Takeda Pharmaceuticals na Global Fund kwa kuunga mkono jitihada za serikali katika kuimarisha huduma za afya kwa mama na watoto wachanga.

Mama Mariam aliwasihii wahudumu wa afya kuwajibika ili kuimarisha afya za wananchi kwa siku za usoni. Alifahamisha kuwa hatua kadhaa zimechukuliwa kupunguza vifo, ikiwemo uchunguzi wa mara kwa mara, kujenga uwezo kwa wafanyakazi, ushirikishwaji wa jamii, na huduma za kina. Mama Mariam alieleza kuwa ZMBF, ilioanzishwa mwaka 2021, imejikita katika

kuchangia maisha bora kwa wanawake, vijana na watoto.

“Kupitia Kampeni za Afya Bora na Maisha Bora, ZMBF inatoa msaada kwa wanawake ambao hawajawahi kuhudhuria kliniki na kuwashauri kuzingatia afya zao,” alisema.

Akimkaribisha mgeni rasmi, Waziri wa Afya Zanzibar, Mhe. Nassor Ahmed Mazrui, alieleza kuwa mradi huo ni nyenzo muhimu ya kuimarisha afya ya mama na mtoto na kupunguza viwango vya vifo, hasa kwa watoto walio chini ya miaka mitano.

Alisema kuwa Wizara anayoiongoza imewekeza katika ushirikiano na vyuo vikuu kama SUZA na LSTM, na mafanikio yao yanaonekana kupitia utekelezaji wa mradi huu huko Unguja na Pemba.

“Majadiliano na maarifa yatakayopatikana katika mkutano huu yatafanyiwa kazi, na mafanikio yetu yatakuwa endelevu,” aliwahakikisha washiriki wa mkutano.

Pia alimpongeza Mama Mariam Mwinyi kwa kujitolea na msaada wake mkubwa katika kuimarisha maisha ya akina mama na watoto kupitia ZMBF.

Katika hafla hiyo, Mh. Mazrui alimkabidhi Mkurugenzi wa Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto wa Tanzania, Dkt. Ahmad Makwani, toleo la Kiswahili la mtaala wa mafunzo ya ANC/PNC.

Makamu Mkuu wa Chuo cha SUZA, Prof. Moh'd Makame

Haji, alitoa shukrani kwa ushirikiano katika programu hiyo ambayo imeleta manufaa mengi kwa jamii kupitia mradi wa huduma za afya Zanzibar.


Alisifu ushirikiano uliosaidia kufanikisha shughuli hizo. Akielezea kuhusu hafla hiyo, Mkuu wa Idara ya Afya ya Umma ya Kimataifa kutoka LSTM, Prof. Charles Ameh, alieleza kuwa lengo la mradi ni kuhakikisha kuwa akina mama na watoto wanapata huduma bora za VVU, TB na malaria katika ANC/PNC.

“Idadi ya watu wanaohudhuria vituo vya afya imeongezeka, lakini tunahitaji zaidi kutoka kwa jamii kote nchini,” alisisitiza.

Katika mkutano huo, tunzo zilitolewa kwa wakufunzi bora na wahudumu wa afya walioonesha mafanikio katika kuimarisha huduma. Vituo vya afya viliviyopata mafanikio makubwa nchini Tanzania, Kenya, na Nigeria pia vilitambuliwa.

Mradi wa Kuimarisha Huduma za VVU, TB na Malaria katika ANC/PNC nchini Tanzania ni mradi muhimu unaolenga kuimarisha afya ya mama na mtoto.

Mradi huu unafadhiliwana Global Fund na Takeda Pharmaceuticals, na unatekelezwa nchini Tanzania (Dodoma na Zanzibar), Kenya, Togo na Nigeria, ukisimamiwa na LSTM kwa kushirikiana na washirika wa ndani katika kila nchi. Nchini Tanzania, wanashirikiana na Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) na Wizara ya Afya (MoH).



## **SUZA yazalisha nguvu kazi ya Taifa - Prof. Haji**

### **Na Mwandishi Wetu, SUZA**

**M**akamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Prof. Moh'd Makame Haji amesema Chuo kina mpango thabiti wa kuwaandaa wahitimu kuwa mchango wa nguvu kazi ya Taifa.

Hayo aliyesema katika ukumbi wa Dk. Ali Mohamed Shein huko makao makuu ya SUZA Tunguu, Mkoa wa Kusini Unguja wakati akizungumza katika mukutano wa ukaribisho wa wanafunzi wapya waliojiunga mwaka wa masomo 2024/2025 kutambua umuhimu wa kuijunga na Chuo kwa kusoma kwa bidii na kwa kujitengenezea uwezo "SUZA tuna jukumu kutoa taaluma katika fani zilizotolewa, Suza haizalishi wasomi wapotevu", Prof. Haji aliaonya wanafunzi hao.

Alifahamisha kuwa mwaka huu wanafunzi 5623 waliomba nafasi za masomo katika fani mbalimbali lakin waliofanikiwa ni 3366 ambapo aliwakumbusha kuwa safari wanayoianza leo inatengeneza misingi ya utegemezi, uongozi na nguvu kazi ya nchi Tanzania.

Prof. Haji aliwapongeza wanafunzi hao wameomba masomo katika ngazi za Astashahada, Shahada na Stashahada na Uzamivu kwa kuwaambia kuwa wamefanya uamuzi bora wa kukichagua SUZA kuwa kichocheo chao cha mabadiliko ya jamii na uchumi wa Zanzibar.

"Dira na dhamira yetu ni kutoa wataalamu ambao watakuwa na faida kubwa si Tanzania pekee bali hata nje ya mipaka", alisitisiza.

Aliongeza kuwa katika kipindi cha miaka 23 iliyopita tangu ilipoanzishwa SUZA, imezalisha wataalamu 18,000 ambao wanendelea kutoa mchango wao katika fani mbali mbali serikalini na sekta binafsi. Naibu Makamo Mkuu wa SUZA anayeshughulikia masuala ya Mipango, Fedha na Utawala, Dk. Hashim Hamza aliaonya wanafunzi wenye tabia ya kuharibu mali za Chuo na kwamba hakuna atakayeachwa kufanya anavyotaka bila kuchukuliwa hatua.

"Hatutomvumilia mwanafunzi yeote atayekiuka nidhamu za Chuo na akibainika atachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria na kanuni za SUZA", alisema Naibu Makamo

Mkuu wa SUZA anayeshughulikia masuala ya Mipango, Fedha na Utawala, Dk. Hashim Hamza. Alifanua kuwa kumekuwa kukiripotiwa uharibifu wa mali kama vile kweenye Dakhalia au kuharibu mali kweenye madarasa kwa kuyunjwa meza za Chuo na mambo mengine ya uharibifu.

"Tunzeni mali za Chuo ili na wengine wakija wavikute vifaa vilivyonunuliwa kwa gharama kubwa vikiwa na hadhi, kwani mkivuruga mtakuwa mmeitia hasara serikali." Alisitisiza Dk. Hamza.

Aidha aliwaonya baadhi ya wanafunzi ambao wanaopewa fedha na wazazi wao lakini kutokana na tabia zao wana hawali-pi fedha hizo na badala yake wanababisha usumbu mkubwa kwa wazazi wao.

"Imekuwa jambo la kawaida kwa baadhi ya wazazi ambao kila unapokaribia wakati wa kufanya mtihani ni lazima wafuatilie watoto wao iwapo wamefikisha ada zao, hii si tabia nzuri", alifahamisha Dk. Hashim.

Aidha aliwakumbusha kuwa Chuo kina Serikali ya Wanafunzi ambapo Changamoto zao zote hufikishwa kwenye uongozi na uongozi huo na wao ndio wanaowajibika kurudisha suluhisho la changamoto hizo baada ya kupatiwa ufumbuzi.

Naye Mkurugenzi wa Shahada za Awali SUZA-DUS, Dk. Khamis Haji, xalisema wazazi wao wamejenga matumaini makubwa baada ya wao kupa fursa ya kuijunga na Chuo.

Hali kadhalika, Mlezi wa Wanafunzi, Bi Salha Khalfan, aliwakumbusha wanafunzi kutumia mitandao kwa ajili ya masomo badala ya kuitumia kwa masuala yao binafsi kwani hawatafaidika na fursa hii na hawatofikia lengo la SUZA kuitumia fursa hiyo kwa ajili ya kuijapatia elimu.

Wanafunzi hao ambao watajiunga katika Kampasi tisa (9) za SUZA wanendelea na vikao yya ukaribisho kwa muda wa wiki moja wakiwepo SUZA na kwenye vituo vyao vya masomo.

## **Mradi wa Upanuzi wa SUZA Wazinduliwa**

### **Na Mwandishi Wetu, SUZA**

**C**huo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kiko mbioni kushuhudia ukuaji mkubwa kupitia mradi wa upanuzi mkubwa unaotarajiwa kuanza Juni 2025 na kukamilika ifikapo mwaaka 2027.

Mpango huu kabambe unahusisha ujenzi wa majengo ya utawala, majengo maalum kwa Skuli ya Elimu na Lughaa, nyumba za wafanyakazi, vituo vya michezo kwa wanafunzi, pamoja na ununuzi wa vifaa vya kisasa na samani, hatua inayoashiria dhamira ya SUZA kuboresha miundombinu na huduma zake.

Katika hafla ya uzinduzi iliyofanyika Hoteli ya Golden Tulip huko Kiemebe Samaki tarehe 19 Oktoba 2024, Makamu Mkuu wa SUZA, Prof. Moh'd Makame Haji, alitangaza kuwa mradi huo unafadhiliwa na Benki ya Kiarabu ya Kiuchumi ya Maendeleo ya Afrika (BADEA) kupitia uwekezaji wa kuvu-

tia wa dola bilioni 14 za Kimarekani. Mkuu wa Idara ya Mikopo na Utawala wa BADEA, Bw. Mohammed El Moctar, alisitisiza mpango wa kimkaati wa benki hiyo kwa nchi za Afrika chini ya dira yake ya mwaka 2030, ambao unalenga kuimarisha miradi ya maendeleo katika miundombinu, kili-mo, biashara, na mipango inayowalen-ga vijana na wanawake.

Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Makungu Juma Makungu, alizindua mradi huo huku akikazia dhamira thabiti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuinua kiwan-go cha elimu.

"Serikali imedhamiria kuboresha vi-wango vya elimu na kuimarisha miundombinu, ikizingatia hasa mazingira bora kwa elimu ya juu," alisema.

Taarifa hii imefafanuliwa kwa ufasha ili kuhakikisha inabeba maana yote muhimu. Tafadhalii niambie ikiwa una-hitaji marekebisho yoyote zaidi.



## SUZA yawahamasisha wadau kuimarisha Mpango wa BSU4

**Na Mwandishi Wetu, SUZA**

**C**huo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kime-wataka wadau kushiriki kikamilifu kwenye Awamu ya Nne ya mradi wa Kujenga Chuo Kikuu Imara (Building Stronger University - BSU4) ili kuimari-sha uhusiano na jamii ya wenyeji.

Katika mkutano na wadau uliofanyika Hoteli ya Golden Tulip Uwanja wa Ndege, Kiembe Samaki, Makamu Mkuu wa SUZA, Prof. Moh'd Makame Haji, alisitisiza jukumu muhimu la wadau katika kufanikisha miradi inayolenga kuboresha elimu, afya, na uendelevu wa mazingira.

“Mkutano huu unatoa fursa kwa wadau kutoa maoni yao, na kusaidia kuboresha mipango ya utekelezaji wa mradi wa BSU4,” alisema Prof. Haji.

Alionyesha umuhimu wa ushirikiano kati ya Chuo na wadau katika kushughulikia changamoto muhimu zinazothiri jamii, huku wakikuza maono ya SUZA ya ubora wa utafiti na huduma kwa umma.

Lengo kuu la mradi wa BSU4 ni kushughulikia changamoto

za afya ya umma, hasa magonjwa yanayoenezwa na mbu. Chuo kinahamasisha mpango wa kuingilia kati maskulini kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Ma-funzo ya Amali, ili kuwafundisha wanafunzi wado-go kuhusu magonjwa haya.

Lengo ni kuwawezesha watoto kuwa na maarifa ili wawe wate-tezi wa suluhisho za kijamii.

“Kwa kuwaelimisha vijana wetu, tunawekeza katika mustakabali ambapo wanawenza kusaidia kulinda jamii zao dhidi ya vitisho vya kiafya,” Prof. Haji aliongeza.

Juhudi nyingine kubwa ni utafiti wa watafiti wa SUZA kuhusu athari za uchafuzi wa bahari, hasa uchafuzi wa mafuta, kwenye mifumo ya iko-lojia ya pwani ya Zanzibar.

Utafiti huu ni muhimu kwa kuhifadhi bayoanuwai tajiri ya bahari ya kisiwa hiki.

“Kuelewa unyeti wa mazingira yetu ya baharini ni muhimu kwa juhudzi za uhifadhi,” Prof. Haji alibainisha, akithibitisha tena kujitolea kwa SUZA katika uendelevu wa mazingira.

Mratibu wa Mradi wa BSU4, Prof. Hamad, aliongeza kuwa maoni ya wadau ni muhimu kwa mafanikio ya mradi.

“Maoni ya wadau yatatusaidia kuimarisha uwezo wa utafiti wa SUZA, kuchochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi, na kuathiri sera,” alisema Prof. Hamad.

Mradi wa BSU, ulioanzishwa miaka 12 iliyopita chini ya uongozi wa Chuo Kikuu cha Copenhagen, ulijumuisha vyuo vikuu 11 mwanzoni.

Leo, SUZA ni moja ya vyuo vi-kuu vitatu vya Kusini vinavyo-endelea na mpango huu, pamoja na Chuo Kikuu cha Gulu nchini Uganda na Chuo Kikuu cha Hargeisa nchini Somalia.

Hili linaonyesha jukumu linaloongezeka la SUZA kama ki-ongozi wa utafiti katika kanda.

Kwa kujitolea kwake kwa suluhisho zinazotokana na jamii, mradi wa BSU4 unawakilisha mwanga wa matumaini, ukionyesha jinsi elimu, utafiti, na ushirikiano wa umma vinyoyeweza kushirikianakushughulikia changamoto halisi za dunia.



## SUZA, ZAWA kufaidika na Cagliari

### Na Jaku Ali, SUZA

**N**aibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Mipango, Fedha na Utawala, Dk. Hashim Hamza Chande, amesema ushirikiano baina ya SUZA, Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) na Chuo Kikuu Cagliari cha Italia umekuja wakati muafaka hasa ikizingatiwa kuwa Chuo kinatarajia kutekeleza mradi wa upanuzi wake hivi karibuni.

Akizungumza tarehe 31 Oktoba, 2024 katika kikao cha pamoja cha maofisa wa ZAWA na wa Chuo cha Italia hapo makao makuu ya SUZA Tunguu katika Mkoa wa Kusini Unguja alisema upanuzi wa Chuo utakuwa na mahitaji makubwa ya maji jambo linalopasa kuwepo ushirikiano na ZAWA na wataalamu wengine ili kuiwezesha huduma hiyo kupatikana kwa ufanisi.

“Kama hatutawashirikisha ZAWA katika jambo hili tutakabiliwa na changamoto za upatikanaji wa huduma hii”, alisema.

Aidha, aliongeza kuwa huu ni mradi muhimu kwa visivu vya Unguja na Pemba ambavyo vinatumia kwa kifwango kikubwa maji ya ardhini.

Naye, Prof. Mshiriki wa Chuo kikuu cha Cagliari cha Italia, Stefania Da Pelo alisema wamezungumza sana kuhusu kuunga mkono na kubadilishana uzoefu katika masuala ya upatikanaji wa maji Zanzibar. Aliongeza kuwa kuna fursa nyinigi za kubadilishana uzoefu na wanafunzi wa vyuo hivi viwili.

Akizungumza katika kikao hicho, Mkurugenzi Mtendaji wa ZAWA, Dk. Salha Khamis Mohammed alisema ameridhishwa sana kuanzishwa ushirikiano huu ambao utachangia kufuatilia kwa ukaribuu mwenendo wa maji Zanzibar.

Aliongeza kuwa wakati umefika kutambua kiwango cha maji kinachopatikana katika ardhi Unguja na Pemba, ubora wake, wapi yameanzia na njia gani yanaelekea.

Naye, Dk. Abdallah Ibrahim, Mhadhiri mwandamizi wa SUZA amesema Italia ni nchi ambayo imeneedlea na ina uzoefu mkubwa katika teknolojia na masuala ya maji. Aliongeza kuwa kutokana na ushirikiano uliopo, SUZA na ZAWA zitafaidika hasa katika kujengewa uwezo na taaluma.

“Sisi tutajifunza kutoka kwao ili kukabiliana na kasi ya

ongezeko la idadi ya watu, na mabadiliko ya tabia nchi”,

“Tusipofanya jambo leo tutakabiliwa na changamoto kesho (miaka 50 ijayo)”, alisitisiza.

Aidha, mazungumzo hayo yatafuatiwa na utiaji saini wa mkataba wa ushirikiano baina ya vyuo hivi viwili. Vyuo vikuu vya Cagliari Italia na SUZA cha Zanzibar vinashirikiana katika tafiti mbali mbali zinazohusiana na maji huku wakishirikiana na Wizara inayosimamia ustawi wa upatikanaji maji hayo chini ya Mamlaka ya ZAWA.

## SUZA, Mkandarasi wasaini Mkataba wa Ujenzi

### Na Jaku Ali, SUZA

**C**huo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kimeingia mkataba na kampuni ya Mohamed Builders Limited kwa ajili ya ujenzi wa majengo mawili: moja kwa Skuli ya Kilimo na jingine kwa ajili ya maabar.

Hafla ya kusaini mkataba huo, iliyofanya tarehe 4 Novemba 2024 katika makao makuu ya SUZA kwenye Kampasi ya Tunguu, Mkoa wa Kusini Unguja, ilihudhuriwa na Makamu Mkuu wa SUZA, Prof. Moh'd Makame Haji, na Bw. Nizar Lakhani, mkandarasi anayewakilisha Mohammed Builders Limited kutoka Dar es Salaam.

Ujenzi huo unaatarajiwa kuanza hivi kari-buni na unatarajiwa kukamilika ndani ya miezi 18, kwa gharama inayokadirisha kuwa dola milioni 20 za Kimarekani.

Akizungumza katika hafla hiyo, Prof. Haji alisitisiza dhamira ya SUZA ya kuchangia maendeleo ya kitaifa kuititia elimu ya nguvu kazi yenye ujuzi.

Alielea kuwa mpango huu unatokana na utafiti wa serikali ulioonyesha upungu mkubwa wa wahitimu, hali iliyosababisha kutolewa mkopo wa dola milioni 20 kujadili maeneo mbalimbali ya utekelezaji wa mradi huo.

“Mradi huu ni uwekezaji katika elimu, ukilenga maboresho makubwa ya, mividombini, mitaala, na uimarishaji wa uwezo kwa wahitimu wa ngazi za ujamili na uzamivu, huku ukizingatia matumizi ya

mifumo ya kisasa ya TEHAMA,” alisema Prof. Haji.

Aliongeza kuwa utekelezaji wa mradi huo unapa swa kuzingatia uzalendo na maslahi ya vijana, kwani ujenzi huo utanufaisha si SUZA pekee bali pia vijana wengi wanatafuta elimu kwa ajili ya kujenga maisha yao na kuchangia maendeleo ya taifa.

Prof. Haji alionya dhidi ya changamoto zozote zinazowenza kuzuia maendeleo ya mradi huo na kuwataka wahusika wote, wakiwemo washauri elekezi, kuhakikisha utekelezaji unafanyika kwa ufanisi.

“Tusijiangushe serikali, viongozi, na wananchi wanaoiajimi serikali yao. Jukumu hili ni la pamoja, na utekelezaji wake unalingana na Ilani ya Uchaguzi ya 2025,” alisitisiza.

Bw. Lakhani, mkuu wa Mohammed Builders Ltd., alihakikishia hadhira juu ya utayari na ufanisi wa kampuni yao, akitaja uzoefu wao mkubwa katika kazini za ujenzi. “Tumejandaa kikamilifu; tukipewa ruhusa leo, kesho tunaanza kazini kwa ufanisi mkubwa,” alisema kwa kujamini.

Mshauri elekezi wa mradi huo, Bw. Lazaro Peter kutoka Arques Africa Ltd., aliwakumbusha wakandarasi umuhimu wa kujitolea kikamilifu kwa mafanikio ya mradi huo. Alibainisha kuwa Zanzibar ina historia nzuri ya miradi iliyofanikiwa na kuwataka waendeleze rekodi hiyo. “Tusijikwa hatua ya kwanza; tuna safari ndefu ya miezi 18 imbele. Tukisema kesho, iwe kweli kesho,” alisitisiza mshauri huyo.



## SUZA, ZBC kushirikiana kuinua tasnia ya habari

**Na Mwandishi Wetu, SUZA**

**C**huo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) na Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC) kuanzia sasa watashirikiana kuimarisha taaluma ya habari na utangazaji kwa kuinua vipaji vya watendaji wao kuwawezesha kufanya kazi katika viwango vinavyokubalika kisekta.

Hatua hii ilifikiwa kufuatia kuwepo kwa pengo katika tasnia hii ambapo matarajio ya vijana wanaoteuliwa kufanya kazi kwa vitendo hayakidhi vigezo vinavyotakiwa katika tasnia hii.

Makamu Mkuu wa SUZA Prof. Moh'd Makame Haji na Mkurugenzi Mtendaji wa ZBC, Bw. Ramadhan Bukini walifikia makubaliano hayo kufuatia mazungumzo yaliyofanyika ofisi za Makao Makuu ya SUZA Tunguu Mkoa wa Kusini Unguja tarehe 26 Machi, 2025 yaliyowashirikisha wanataaluma wa SUZA na watendaji kutoka ZBC.

Katika mkutano wa viongozi hao, walikubaliana kutengeneza vijana mahiri ili kuepusha wimbi la vijana waliokuwa tayari kufanya kazi kwa kujitolea wasiokidhi viwango.

“Tangu tumefanya mabadiliko ya mfumo ZBC miaka miwili iliyopita, tumeona kuna pengo kati ya mahitaji ya soko kwenye taaluma wanazokuja nazo kutoka vyuoni, tumetengeneza namna ya wanafunzi wengi zaidi kuja kupata uzoefu ambaeo utakuwa wazi mwaka mzima”, alisema Bukini.

Alisema ili kukabiliana na hali hiyo shirika lina mkakati wa kuwachukua vijana wengi zaidi kwenye mazoezi ya vitendo hali ambayo itachangia kuleta ufanisi wakati watakapokuwa tayari kuanza ajira rasmi.

“Umfikia wakati tutengeneze vijana wenye ujuzi, akisimama mtu akizungumzia suala fulani au akifanya mahojiano na mtu mwengine mtaalamu na yeze anapaswa kuwa na utaalamu wa jambo hilo badala ya kugusia gusia tu juu juu”, alifahamisha.

Makamu Mkuu wa SUZA Prof. Haji alisema amefarajika kwa ZBC kutaka kushirikiana na SUZA katika sekta hii na kusema kuwa ana matarajio makubwa ya kupatikana ufanisi.

Alisema SUZA itaendelea kuongeza wigo wa kuwa na

programu mpya za masomo ambazo zitaanza kutumika rasmi mwezi Oktoba mwaka huu huku matarajio ya kuongeza wanafunzi wapya yanakadirwa kufikia 1,500 mwakani.

Aliongeza kuwa taasisi anayoiongoza inajikita kutekeleza sera, dira, mipango mikuu ya maendeleo kufanya tafiti na kuendelea kuandaa wataalamu ambaeo ndio wanaotumika katika taasisi mbalimbali nchini.

Katika mazungumzo hayo, Prof. Haji ameagiza kuanza kutekelezwa mara moja kwa kuandaliwa hati ya makubaliano itakayowaongoza kutekeleza majukumu yao kisheria na kwa ufanisi.

Ushirikiano wa mashirika hayo mawili, unatarajiwa kuwajengea uwezo wanafunzi katika Skuli ya Habari na watendaji katika idara za habari za SUZA kwa kufanya kazi kwa kujitegemea zaidi mfano mtu mmoja kupiga picha na kuihariri, kuandika habari na kuihariri, mtangazaji na mtengenzaji wa vipindi, na mtendaji ambaye atashughulikia masuala ya mitando ya jamii na kubadilishana wataalamu katika sekta hiyo kwa tasi za habari za ZBC.



## Wahitimu program mpya watunukiwa Shahada SUZA

**Na Jaku Ali, SUZA**

**M**akamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Prof. Moh'd Makame Haji amesema Chuo kimeanzisha program mpya ya Shahada ya Tabibu Kinywa na Meno (Bachelor of Science in Doctor of Dental Surgery) ambapo kwa mara ya kwanza wahitimu watano wametunuliwa Shahada zao.

Akitoa salamu zake katika Mahafali ya 20 yaliyofanyika katika makao makuu ya SUZA Tunguu, Mkoaa wa Kusini Unguja, Prof. Haji alisema kati ya wahitimu hao watano wanawake ni wawili na wanaume ni watatu.

“Wahitimu hawa si tu wanawakilisha matunda ya kazi yetu ya pamoja, bali pia ni alama ya matumaini kwa maendeleo ya Zanzibar na nchi yetu kwa ujumla”, alifafanua Prof. Haji.

Akizungumzia kuhusu ongezeko la wanafunzi kwa ujumla alieleza katika mwaka huu, alisema kumekuwa na ongezeko kubwa la wahitimu wanawake wanaofikia asilimia 61 ikilinganishwa na wahitimu wanawake waliofikia asilimia 58.46 mwaka 2023.

Akitoa ufanuzi zaidi alisema kati ya wahitimu 2,291 mwaka huu, wahitimu 6 (3 wanaume na 3 wanawake) walitunukiwa Shahada ya Uzamivu, wahitimu 73 (26 wanaume, 47 wanawake) walitunukiwa Shahada za Uzamili, wahitimu 791 (323 mme, 468 w'ke) walitunukiwa Shahada za Kwanza, wahitimu

1095 (389 wanaume, 706 wanawake) walitunukiwa Stashahada, na wahitimu 322 (143 wanaume, 179 wanawake) walitunukiwa Astashahada (cheti).

Kutokana na mafanikio hayo SUZA itakuwa imezalisha wahitimu zaidi ya 19,000 tangu ilipoanza kazi ya kutoa taaluma miaka 24 iliyopita.

Aidha, alitumia fursa hiyo kwa niaba ya wafanyakazi wa SUZA

## APRM kuwafungulia fursa wanataaluma SUZA

**Na Mwandishi Wetu, SUZA**

**M**akamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Prof. Moh'd Makame Haji amepokea wazo la kushirikiana na Mpango wa Hiari wa Nchi za Umoja wa Afrika Kujipima kwa Vigezo vya Utawala Bora (APRM) utakaongeza kasi ya utekelezaji wa dhana hiyo kuwaongezea ujuzi wanataaluma kwa kushirikiana na wadau wengine katika kutoa elimu.

Hatua hiyo imefikiwa katika kikao kilichowakutanisha watendaji wa APRM na SUZA kilichofanyika tarehe 27 Machi, 2025 Makao Makuu ya SUZA Tunguu Mkoaa wa Kusini Unguja kilichojadili namna watakavyoweza kufanya kazi kwa pamoja.

Akizungumza katika kikao hicho, Prof. Haji alisema ushirikiano wao ni fursa muhimu kwani SUZA nayo itaweza kusikika na kubadilishana uzoefu kwa kufanya kazi na taasisi nyengine.

“Chuo kinaendeshwa kwa vigezo vya Kamisheni ya Vyuo Vikuu vya Tanzania (TCU) na ubora ukishuka vigezo vinakukamata na kukulazimisha kutotumia programu fulani hadi urekebele halii hiyo”, alisema Prof. Haji.

Alieleza kuwa, kumekuwa na matokeo mazuri ya utekelezaji wa majukumu

kuwapongeza wahitimumu wote kwa jitihada zao hadi kumaliza masomo yao kwa salama.

“Ningependa kusema kwamba leo si mwisho wa safari ya elimu, bali ni mwanzo wa safari mpya. Wahitimu mnaendelea kuwa na jukumu la kuleta mabadiliko kwenye jamii yetu, taifa letu, na ulimwengu kwa ujumla”, alisisitiza Prof. Haji

ya SUZA kutokana na kufanya tathmini kila baada ya miaka mitano ambapo tathmini ya mwisho ilifanyika mwaka 2025 na Chuo kilipewa hati ya kuendelea na shughuli zake.

Aidha, aliongeza kuwa kwa vile ni Chuo cha Umma kina mamlaka kadhaa zinazofanya tathmini ikiwa ni pamoja na Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi na miradi ya maendeleo ya mashirika ya kimataifa pia ina wakaguzi wake.

Naye Mjumbe wa Baraza la Taifa la Usimamizi la APRM Bw. Said Ali Mussa, alisema taarifa za APRM hujadiliwa na wakuu wa nchi wa Umoja wa Afrika (AU) ambazo huangalia maendeleo yaliyofikiwa, changamoto na namna gani zinazovoyeweza kupatiwa suluhu.

Katika mpango huo ambapo Tanzania ilijuunga rasmi mwaka 2004 nchi ziliona umuhimu wa kuwa na chombo ambacho kitatoa tathmini kwa nchi wanachama wa umoja huo badala ya kuyaachia mataifa mengine kufanya kazi hiyo kwa vigezo vyao.

Akizungumza katika kikao hicho, Katibu Mtendaji alipendekeza kuwa taasisi hizi ni vyema zikawa na mahusiano ya kudumu ambapo taasisi ya APRM inaweza kuchangia kutolewa miadhara kwenye masuala ya utawala bora kwa kuleta wataalamu.



## Jamii yaelekezwa kuwahimiza vijana kusoma

### Na Mwandishi Wetu, SUZA

Serikali ya Wanafunzi ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) imefanya ziara katika Shehia ya Kidoti iliyoko Mkao wa Kaskazini ‘A’ Unguja. Lengo la ziara hiyo lilikuwa ni kutoa sadaka kwa wanavijiji wa shehia hiyo pamoja na kuhimiza umuhimu wa elimu katika maendeleo ya jamii. Kujitolea kwa wanafunzi hao kunaonesha nguvu ya vijana katika kuleta mabadiliko chanya.

Katika ziara hii, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Prof. Moh'd Makame Haji aliambatana na wanafunzi hao na kutoa wito kwa jamii kuwahamasisha vijana kuchangamkia fursa za masomo kuanzia ngazi za chini ili kutengeneza mazingira ya kujiunga na elimu ya juu.

Alisema katika kuwawezesha vijana kufikia malengo ya kupata elimu bora, Sera ya Elimu ya Tanzania imefanyiwa marekebisho huku Sera ya Elimu ya Zanzibar inakamilishwa kufanyiwa marekebisho ili kutoa fursa kwa watoto kujipatia elimu itakayoweza kuwajengea mustakabali mwema wa maisha siku zizazo.

“Mabadiliko haya yatawasaidia vijana wanaojifunza elimu za kawaida na elimu za amali au vitendo kufanya kazi za ujuzi katika sekta mbalimbali”, alisisitiza.

Alisema chuo kinatoa fursa

kupitia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa vijana kupata mikopo kupitia Bodi za Mikopo za Tanzania na Zanzibar kujiunga na masomo na pia kupata ufadhili kupitia Mama Samia Scholarship. “Kwa ufadhili wa Mama Samia, wanafunzi anadhaminiwa kila kitu, yeze apate ujuzi tu akirudi afanye kazi”, alikumbusha. Aliongeza kuwa wazazi wanafanya jitihada kuwapatia mahitaji ya msingi vijana na wao wanapaswa kukazania kusoma ili wawe wataalamu kwenye fani mbalimbali zinazohitaji ujuzi. “Hata kazi za kawaida tulizozirithi kwa wazee wetu nazo zinahitaji utaalamu”, alisisitiza.

Aidha, alitoa mfano wa kazi ya uvuvi ama kulima mwani ambazo pia zinahitaji utaalamu. “Badala ya mashua zinatumika boti zinazotumia mashine ama za jua au za mafuta na endapo utakaosekana utalaamu wa matumizi ya vifaa vya kisasa uzalishaji wake pia utakuwa duni”, alisema Prof. Haji.

Hata hivyo, alizungumzia changamoto inayowakabili wanafunzi wa Zanzibar ya kukatisha masomo kutohana na sababu mbali mbali hali inayowakosesha fursa vijana kwani ulimwengu kadri unavyoendelea unahitaji wabobezi katika taaluma mbalimbali.

Aliongeza kuwa katika kuwaweka mazingira bora ya elimu ya juu, Chuo kinaendelea

kuweka miundo mbinu bora ya kisasakamavilemajengo, maabara za kisasa, mifumo ya TEHAMA, na walimu wanaoenda sambamba na mahitaji ya wanafunzi.

Aidha, kuhusiana na lengo la ziara hiyo, Rais wa Serikali ya Wanafunzi, Bi Mwanamkuu Jega Bakari aliushukuru uongozi wa chuo kwa kuiunga mkoni serikali yake katika kuwasaidia wananchi katika kupindi hiki.

Aliongeza kuwa, ugawaji wa sadaka kila mwaka ni utamaduni wa serikali ya wanafunzi hali inayowaweka karibu wao na jamii. Jambo linalowawezesha kutambua changamoto na kupata suluhisho la kutatta changamoto zao kupitia tafiti na mazungumzo yanayofanyika baina yao.

Nao wanavijiji wa shehia hiyo, wamefurahia kukumbukwa na SUZA na wameziomba taasisi nyengine ziige mfano kama huo, hata kama siyo kipindi cha mwezi mtukufu wa Ramadhani.

Sheha wa Shehia hiyo, Bw. Hamad Makame Haji, alitoa wito kwa watu wengine kuzisaidia familia zenye mahitaji maalumu ili nazo ziweze kuishi kwa furaha na matumaini.

Wakaazi wengine wa shehia hiyo; Bw. Bakari Machano Juma na Bi. Hawa Juma nao pia walitoa shukurani zao kwa SUZA na kuwaomba siku nyengine wawakumbuke tena kwa kuwapatia sadaka.



## Kongamano la Utafiti wa Elimu 2025 lafungwa

### **Na Mwandishi Wetu, SUZA**

**K**ongamano la siku mbili la Utafiti wa Elimu Tanzania 2025 lililoandaliwa na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kwa ushirikiano na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) limefungwa rasmi tarehe 26 Februari, 2025.

Akifunga kongamano hilo, katika ukumbi wa SUZA Kampasi ya Maruhubi tarehe Naibu Katibu Mkuu Taaluma wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali,

Dkt. Mwanakhamis Adam Ameir alisema mijadala iliyofanyika katika mukutano wa Utafiti wa Elimu italeta tija iwapo itatekelezwa kwa vitendo kumaliza changamoto zinazozikibili sekta ya elimu.

Alifahamisha kuwa anaamini mada zote zilipata wachangiaji wazoefu kwenye sekta ya elimu na kwamba wataweza kuleta mabadiliko makubwa ya elimu na kufikiwa malengo yaliyokusudiwa.

“Mafunzo yaliyotolewa katika kongamano hilo yamekusudiwa kufanyiwa kazi kwa vitendo ili kuondokana na shida zilizopo na kufikia malengo yanayotakiwa”, alisema.

Katika kongamano hilo, mada nne zilijadiliwa ikiwa ni pamoja na maandalizi ya walimu, mitaala na mazingira, tatizo la wanafunzi kuacha masomo, na utafiti na ubunifu ambazo zilijadili kwa kina maendeleo na changamoto zilizopo katika sekta hiyo.

Akizungumza katika hafla hiyo, Kamishna wa Elimu Tanzania Prof. Lyambwene Mtahabwa alitoa shukrani kwa wadau wote wa elimu wa ndani na nje ya Tanzania kukamilisha vyema kongamano hilo.

Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kimeshirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wa Kongamano la Utafiti Elimu Tanzania 2025 ambalo limewajumuisha

washiriki zaidi ya 500 wakiwemo wasomi, watunga sera, na wadau wa elimu kutoka ndani na nje ya nchi.

Lengo la kongamano hilo ni kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika elimu, kuendeleza programu za mafunzo endelevu kwa walimu na watafiti, na kuhakikisha matokeo ya tafiti yanatumika katika utengenezaji wa sera bora za elimu.

## **Baraza la Chuo lakutana na wanataluma**

### **Na Mwandishi Wetu, SUZA**

**M**wenyekiti wa Baraza la Chuo Cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) Bi Hamida Mohammed Ahmed amesema utekelezaji majukumu ya Baraza umechangia kuweka mazingira mazuri ya utoaji wa huduma za Chuo.

Akizungumza katika mukutano wa pamoja na wanataluma na wajumbe wa Kamati mbalimbali za SUZA uliyofanyika Makao Makuu ya SUZA Tunguu Mkoo wa Kusini Unguja tarehe 28 Januari, 2025, alisema SUZA imekuwa na mabadiliko makubwa katika utoaji wa elimu na kuimariswa miundombinu ya Chuo.

Aidha, aliwashukuru wajumbe wa Baraza la Chuo na wanataluma kwa ushirikiano mkubwa wanaouonesha unaochangia kufanikisha malengo yaliyowekwa na kuahidi kuwa mukutano kama huu utakuwa wa kudumu kwa ajili ya kutuatua changamoto zinazojitokeza.

Mapema, Makamu Mkoo wa SUZA, Prof. Moh'd Makame Haji alifahamisha kuwa SUZA inashirikiana na wadau mbalimbali

wakiwemo watalamu kutoaka Kamisheni ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), na vyuo vyenye sifa na uzoefu mkubwa katika utoaji huduma.

“Tunatengeneza mazingira rafiki yatakayokivusha Chuo hatua nyengine ya mafainikio, ifahamike kuwa baadhi ya mambo yanayofanywa na SUZA ni lazima yapite Serikali kuu kabla ya kutekelezwa”, alikumbusha.

Alisema pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana, suala la tafiti linahitaji kuwekewa mkazo mkubwa.

Naye Mwenyekiti Kamati ya Ustawi ya SUZA, Bi Salma Saadat, alipendekeza kuwa wanafunzi washajiishwe kuwasilisha changamoto zao katika Kamati za Ustawi za Chuo.

Rais wa Serikali ya Wanafunzi ya SUZA (SUZASO), Mwanamkuu Jega aliwashauri wanataluma kutumia lugha za busara kwa wanafunzi wanapotoa maelekezo. Alithibitisha kuwa wako tayari kuongozwa na wanataluma kwani wao ni watu wa mwanzo wanaoshuhudia mwanzo maendeleo yao ya elimu.



## SUZA yawaandaa viongozi mahiri

### Na Mwandishi Wetu, SUZA

**N**aibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee Wanawake na Watoto Mhe. Anna Athanas Paul amesema Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kinawaandaa viongozi mahiri watakaoweza kusimamia mipango na mikakati mkuu ya nchi siku zijazo.

Akitoa hutuba ya maadhisho ya Siku ya Ustawi wa Wanafunzi yaliyoandaliwa na Serikali ya Wanafunzi ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) yaliyofanyika Taasisi ya Utalii huko Maruhubi Kampasi ya SUZA, Mhe. Anna alisema ameridhishwa na utekelezaji wa majukumu ya SUZASO unaaoonesha umahiri na ukomavu kwa viongozi wake.

Alitaja mionganini mwa mambo yaliyomvutia ni uongozi kuunda Wizara Ustawi wa Wanafunzi ili kutoa fursa kwa shughuli zinazohusuustawikushughulikiwa na wanafunzi wenyewe badala ya Wizara inayoshughulikia watu wenyewe ulemavu.

“Huu ni ubunifu mzuri na ndio ukomavu wa kimaono wa na huu ndio ushahidi kweli SUZA tunawaandaa viongozi bora na mahirikupitia SUZASO”, alisema.

Akizungumzia kuhusu masuala ya udhalilishaji, alisema dhamira njema ya Serikali ya kuzalisha vijana waliobobe katika taaluma haitaweza kufikiwa iwapo vitendo viovu vya udhalilishaji hasa kwa wanawake na watoto vitaendelea kuwepo na kudhoofisha

malengo ya utoaji elimu bora.

Vilevile alitoa wito kwa wanafunzi kutokaa kimya iwapo kutakuwa na ishara au matukio udhalilishaji na kuwataka kuripoti kwenye mamlaka zilizowekwa kisheria.

Alifahamisha kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Mapinduzi ya Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi imejitahidi katika ujenzi wa miundombinu kama vile skuli za kisasa, uimarishaji wa elimu ya juu sambamba na ujenzi wa majengo mapya ya SUZA.

Mapema, Makamu Mkuu wa SUZA, Prof. Moh'd Makame Haji alisema SUZA inafanya mambo mengi yenye mnasaba na Siku ya Ustawi kwa kutoa elimu bora kupitia programu zake programu 60 za Cheti, Diploma, Shahada, Digirii na Uzamivu.

“Programu zote zinatolewa katika kiwango bora cha kuwawezesha wahitimu kutumia taaluma kuleta mabadiliko na kuchangia maendeleo ya nchi ”, alisisitiza Prof. Haji.

Kuhusu kupambana na udhalilishaji, Prof. Haji alisema Chuo Kikumeweka madawati ya Jinsia katika Kampasi zake zote ambazo zina uwakilishi kwa walimu na wanafunzi kutoa malalamiko yao.

“Chuo Kikuu pia kinatoa elimu kwa wanafunzi 58 wenyewe mahitaji maalum wakiwemo wenyewe uoni hafifu, wasioweza kutembea na kuzungumza na wote wanafanya

vizuri kutokana na mipango mizuri iliyowekwa ya utoaji wa elimu”, alikumbusha Prof. Haji.

Mambo mengine ambayo Prof. aliyataja kuwa ni mafanikio katika ustawi wa wanafunzi ni kuwepo kwa bajeti maalum ya Serikali ya Wanafunzi, kuwashirikisha katika kila matukio ya Chuo kama vile vikao vya juu vya SUZA vya kupidisha maamuzi, kuwashirikisha katika matamasha ya michezo ya ndani na nje ya nchi, kuwawekea vituo vya ujasiriamali, kuangalia mahitaji ya karne ya 21 ya Teknolojia ya kisasa na kuwawekea wanafunzi miundombinu hiyo na kituo maaluma cha kuatamia mawazo ya kibiashara.

Naye Rais wa Serikali ya Wanafunzi ya SUZA, Mwanamkuu Jega Bakari, aliushukuru uongozi wa SUZA kwa kuwasimamia vyema katika masomo na shughuli zao za Serikali yao sambamba na masomo yao.

Katika hafla hiyo, Rais wa Wanafunzi aliiomba Wizara ya maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee, Wanawake na Watoto kushirikiana nayo kwa kupewa mafunzo yanayohusua masuala ya ustawi wa jamii ombi ambalo mgeni rasmi alilikubali.

Naye Waziri wa anayesimamia masuala ya Ustawi wa Serikali ya Wanafunzi, Khatib Nassor alisema kuwa kuwepo kwa Serikali hiyo kumeleta umoja na mshikamano kati ya walimu na wanafunzi wote wa SUZA.



## Dk. Mwinyi atoa wito kutengeneza vijana soko la ajira

### Na Mwandishi Wetu, SUZA

R AIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dk. Hussein Mwinyi ametoa wito kufanyika upembuzi yakinifu wa program za mafunzo ya amali ili kuandaa wahitimu kwa soko la ajira na mahitaji ya viwanda.

Mheshimiwa Rais Mwinyi aliyasema hayo katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mhe. Hemedi Suleiman Abdullah wakati akiwahutubia wadau wa elimu.

Alizitaja rai hizo kuwa ni pamoja na kuongeza ushirikiano kati ya taasisi za Elimu na Sekta Binafsi, ambapo kwa mkakati huo watapatikana wahitimu wenye ujuzi unaotakiwa sokoni.

Nyengine ni kutambua changamoto zinazowakumba vijana, hasa wanawake na makundi maalum katika upatikanaji wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi na kuzipatia suluhisho.

Aliongeza kuwa kuimariswa mitaala ya elimu na mafunzo ya amali ili kuhakikisha kuwa inakidhi mahitaji ya soko la ajira linalobadilika kwa kasi na kufanya utafiti wa matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na teknolojia bunifu.

“Ni matumaini yangu kuwa tafiti katika maeneo hayo zitaiwezesha Serikali na wadau wa elimu kufanya maamuzi sahihi ya kukuza sekta ya mafunzo ya amali yatakayowapatia vijana wa Tanzania ujuzi wa kisasa wa kuchangia maendeleo ya Taifa”, alisema Dk. Mwinyi.

Mapema, Makamu Mkuu wa Chuo cha Taifa cha Zanzibar, Prof. Moh'd Makame Haji alisema SUZA inaongoza kwa kufanya tafiti zinazohusiana na mazingira, afya, elimu, na uchumi ambazo

zimeleta mchangano mkubwa katika kuimariswa sera za elimu na maendeleo Zanzibar na Tanzania kwa ujumla. Aliongeza kuwa makongamano kama hili yanatoa fursa kwa watafiti, wasomi, na watunga sera kubadilishana maarifa na kuimariswa mwelekeo wa utafiti wa elimu.

Akizungumza kwa niaba ya Kamati ya maandalizi katika mukutano huo, Bi. Hannah Simon, alisema Utafiti Elimu Tanzania 2025 ni matokeo ya kazi kubwa ya Kamati ya Maandalizi, inayoongozwa na Chuo Kikuu cha

Taifa cha Zanzibar (SUZA), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kupitia CoICT (UDSM-CICT), Wizara ya Elimu,

### SUZA yaanza kuonesha njia uchumi wa kidigitali

### Na Mwandishi Wetu, SUZA

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Prof. Moh'd Makame Haji amehimiza Chuo kutumia fursa ya kushirikiana na wageni kutoka nchi zilizopiga hatua katika teknolojia ya kisasa ambayo inaendana na sera ya nchi hasa katika kuimariswa uchumi wa kidigitali.

Hayo aliyasema tarehe 10 Januari, 2025 katika ofisi za Makao Makuu ya SUZA wakati akizungumza katika hafla ya mafunzo ya siku tatu kwa wageni kutoka nchi za Jordan, Morocco, na Lebanon, kuhusiana na kuwasaidia wanafunzi wa masomo ya Sayansi kutumia teknolojia ya kisasa.

Alifahamisha kuwa kwa ushirikiano huo, SUZA itazidi kuzalisha wataalamu wengizaidikatikatechnolojiahyoambao watafanya mambo makubwa katika utendaji wa hali ya juu katika kompyuta kwa kufanikiwa kufahamu mambo mengi zaidi yanayoendelea duniani.

Naye Dkt. Maryam Masoud Khamis Mhadhiri wa SUZA katika Idara ya Sayansi ya Kompyuta alisema kuwa Mradi huo uliofadhliliwa na Jumuiya ya Ulaya una lengo la kuwasaidia wanafuzi wa wa Masomo ya Sayansi katika maeneo ambako hakuna teknolojia hii kuweza kuitumia.

Sayansi na Teknolojia, na Taasisi ya Elimu Tanzania (TIE) kwa kushirikiana na FCDO, Canada, British Council, EdTech Hub, na Aga Khan Foundation.

Aidha, katika kongamano hilo mada kuu zilijadiliwa ikiwa ni pamoja na Wanafunzi wanaoacha skuli, wanaobaki na wanaorejea skuli, Maandalizi ya Walimu, Hali ya Hewa, Mazingira na Elimu na Elimu ya Ufundji Stadi (TVET) na Uwezo wa kupata ajira.

Mkutano huo ni wa nne ambapo kwa mara ya kwanza umefanyika Zanzibar, ukiwashirikisha wadau mbali mbali wa elimu kutoka ndani na nje ya Tanzania na ulidhaminiwa na mashirika ya kimataifa na kijamii lakini pia na

Wanafunzi wataweza kuitumia teknolojia hata kama wako maeneo ambayo mtandao huo haupo hali itakayosaidia kupambana na uhaba wa vifaa, kuwezesha kuitumia teknolojia wakati wowote hata kama ni usiku

“Hii ni fursa muhimu kwani itawezesha kupambana na uhaba wa vifaa, kupatikana wakati wowote kwa wanafunzi”, aliezeza

Aliongeza kuwa SUZA inaandaa mtaala wa Usalama wa Mtandaoni kwa Wanafunzi wa Shahada ya Kwanza na Uzamili ambapo jambo hili ni muhimu kwani SUZA inakuwa ya mwanzo kulianzisha. Aliezeza kuwa SUZA imeongeza mwendo kwenye taaluma hii kwani ina kozi za usalama wa kintando kwa wanafunzi wa shahada ya kwanza.

Mafunzo hayo yaliwashirikisha zaidi ya wageni 20 ambapo siku ya mwisho ya ziara walishiriki pia wanafunzi wengine ambao hawakuweza kuwahi. Akizungumzia kuhusu ushiriki wa wanawake katika teknolojia alisema anaona fahari ye ye kuwa mmoja wapo lakini eneo hili limekosa ushiriki mkubwa wa wanawake. Alishauri watumie maabaraka hii vizuri kwani fursa ya watu wengine wasiokuwa wanafunzi wa SUZA pia wataruhusiwa kuitumia.



## SUZA, Whitworth kuimarisha ushirikiano katika programu za Wanafunzi

### Na Mwandishi Wetu, SUZA

**M**kuu wa Idara Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) ya Kiswahili kwa Wageni Bi. Shani Suleiman Khalfan ameushukuru uongozi wa Chuo Kikuu cha Whitworth cha Marekani kwa kuendelea kuichagua SUZA kupokea wanafunzi wake kwa ajili ya kuwasomesha lugha ya Kiswahili.

Alisema huduma hiyo wamekuwa wakiitoa kwa muda wa miaka 10 bila kusita na ana matumaini kuwa wataendelea kuwa pamoja katika kuikuza lugha ya Kiswahili.

Akizungumza katika mahafali ya kupewa vyeti na kuagwa wanafunzi walijifunza katika Skuli hiyo katika Kampasi ya SUZA iliyoko Vuga, Bi Shani aliwashukuru wazazi wa familia walizokuwa wakiishi na wageni kwa kukaa nao vyema.

“Ahsante sana kwa kutuamini, ninaamini kwamba msaada huu hauko kwa walimu tu bali pia wazazi tunawashukuru sana kwa kutusaidia kuishi na wageni wetu vizuri”,

Naye Kiongozi wa Sayansi ya Siasa aliyebolea katika masomo ya Kiafrika Chuo Kikuu cha Whitworth Marekani Prof. Megan Hershey alisema ameridhishwa sana na uongozi wa SUZA kwa kuwawezesha kusoma lugha ya Kiswahili katika mazingira

mazuri ya darasani na familia walizokuwa wakiishi nazo. Akitoa shukurani hizo, Prof. Megan alisema programu za kufundishwa Kiswahili zimekuwa zikiratibiwa vyema kwa muda mrefu na kuahidi kuwa wataendelea kuwa pamoja katika kuendelea kuikuza lugha ya Kiswahili.

Aidha, alizitaja familia ambazo wanafunzi walikuwa wakiishi nazo pia zimetoa mchango mkubwa wa maendeleo yao sambamba na kuwafundisha mambo mengine ya utamaduni wa Mswahili.

Wakitoa shukurani zao katika maonesho madogo madogo ya kuzungumza kama kama michezo ya kuigiza mbele ya wageni katika mahafali

hayo walieleza kufurahishwa kwao na jinsi walivyojifunza na kuishi katika familia.

“Tumefurahi kuwa na uzoefu mkubwa katika lugha, tunadhani Kiswahili chetu kimekuwa kwa mfano hivi sasa tuna uwezo wa kusoma vitabu, tunapambana na tunatarajia tutaweza kufanikiwa zaidi”, alisema mwanafunzi

Katika masomo hayo pia wanafunzi 15 waliohitimu masomo yao ya mwezi mmoja walipata fursa ya kutembelea maeneo mbalimbali ya kihistoria pia maeneo msituwa hifadhi wa Jozani, Jambiani, Kizimbani, Maruhubi na Kijichi, na Nungwi ambamo mote humo walijifunza matumizi ya lugha ya Kiswahili katika uhalisia wake.

## KAMATI YA JARIDA

Mwenyekiti	Ndg. Hassan Simba Hassan
Mratibu	Ndg. Khadija Sadiq Mahumba
Mhariri wa Makala	Dkt. Masoud Nassor Mohammed
Mhariri wa Habari	Dkt. Rashid Maalim Khamis
Mtayarishaji Habari	Ndg. Nasima Haji Chum
Mpiga Mpicha	Ndg. Hamza Makame Ussi
Msanifu Jarida	Ndg. Zedi Abdalla Khamis



## SUZA yafanya uhamasishaji skuli za sekondari bara

### **Na Mwandishi Wetu, SUZA**

**K**atika mkakati wa kuongeza idadi ya wanafunzi wa kujiunga na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) Kitengo cha Uhusiano cha SUZA kwa kushirikiana na Kurugenzi ya Shahada za Awali (DUS) wamefanya ziara ya katika skuli za sekondari za baadhi ya mikoa ya Tanzania bara kwa madhumuni ya kuwapa wanafunzi wa skuli hizo taarifa muhimu kuhusu masharti ya kujiunga na SUZA, programu zinazopatikana, na fursa zinazotolewa na elimu ya juu. Ziara hii ililenga kuwatia moyo wanafunzi na kuwapa maarifa wanayohitaji ili kufanya maamuzi sahihi kuhusu mustakabali wao wa kitaaluma.

Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano cha SUZA Bi. Khadija Sadiq Mahumba alieleza kuwa ziara hizo zilifanyika kuanzia tarehe 24 Februari, 2025 hadi 28 Februari, 2025 ambapo mikoa iliyotembelewa ni Mkoa wa Mtwara uliotembelewa skuli zilizopo manispaa ya Mtwara; mikoa mingine ni Lindi, Morogoro na Singida ambapo jumla ya skuli sabini na sita (76) ndani ya mikoa hiyo zilipata fursa hii adhimu ya kutembelewa na maafisa mbalimbali waudahiliwa SUZA.

Kwa mujibu wa Bi. Khadija Mahumba, malengo mahsusii ya ziara hiyo yalikuwa ni kuwapa wanafunzi taarifa kuhusu sifa za kujiunga na SUZA na programu zinazopatikana,

kueleza mchakato wa maombi na muda wake, kuwapa wanafunzi mtazamo wa maisha ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, udhamini wa masomo, na fursa za taaluma.

Hatimaye wanafunzi wote wa skuli zilizotembelewa walipata fursa ya kuuliza masuali ambayo mengi yao yalilenga kufahamu kuhusu kozi, ada za masomo, udhamini wa masomo, na maisha ya chuo kikuu. Aidha wanafunzi walihitaji kupata ufanuzi wa masharti ya kujiunga, vigezo vya uteuzi, na mchakato wa maombi.

Masualiyotehayoyalijibiwakwa ufasaha na maafisa wa SUZA, alieleza Bi. Khadija Mahumba. Katika baadhi ya skuli zilizotembelewa wanafunzi wengi walionesha shauku ya kujiunga na SUZA lakini walikosa maarifa kuhusu vigezo vya uandikishaji.

Aidha walionesha wasiwasi kuhusu changamoto za kifedha na fursa za ufadhili wa masomo, changamoto hizo zilipatiwa ufanuzi na maafisa hao wa SUZA na kuwatoa wasiwasi wanafunzi kwa kuwaeleza kuwa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) ni mkombozi mkubwa wa changamoto hizo za wanafunzi kwa wale watakaoomba mikopo hiyo.

Katika uimarishaji wa ufahamu kwa wanafunzi hao kuhusu maisha yao yatakavyo kuja kuwa ndani ya Chuo baada ya

kujiunga, vipeperushi vyenye miongozo vilitolewa kwoo.

Maafisa wa SUZA waliwahamasisha na kuwataka wanafunzi hao kufanya bidii na kuwanamalengoya elimu yajuu.

Nao walimu wa skuli zilizotembelewa walikuwa na mawazo yanayofanana ya kuwataka maafisa wa SUZA kufanya ziara za mara kwa mara katika skuli zao kwa lengo la kutoa elimu kwa wanafunzi wao kuhusiana na mahitaji ya kujiunga na SUZA.

Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar katika miaka ya hivi karibuni kimekuwa kikipokea wanafunzi wengi kutoka Tanzania bara kutokana na ziara za namna hii ambazo kufanya kila mwaka katika mikoa mbalimbali ya huko.

Jumla ya mikoa mitatu ambayo ni Arusha, Mwanza na Tabora ilitembelewa kabla ya kuanza kwa mwaka huu wa masomo kwa lengo la kuongeza idadi ya wadahiliwa.

Baadae katika mwaka huu wa masomo SUZA inatarajia kutembelea skuli zote za sekondari katika mikoa yote ya Unguja na Pemba.

Ziara hizi zimesaidia kuongeza idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa na SUZA kwa kila mwaka ambapo mwaka wa masomo 2023/2024 udahili wa wanafunzi wapya uliongezeka kwa asilimia nane.

Picha za matukio mbalimbali katika sherehe ya Mahafali ya 20 ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) yalifanyika tarehe 28 Disemba, 2024 katika Ukumbi wa Dkt. Ali Mohamed Shein Tunguu Zanzibar



*Photos of various events at the 20<sup>th</sup> Graduation Ceremony of the State University of Zanzibar (SUZA) held on December 28<sup>th</sup>, 2024 at the Dr. Ali Mohamed Shein Hall - Tunguu Campus Zanzibar*





## SUZA conducts awareness campaign in Mainland Secondary Schools

By Our Reporter, SUZA

As part of its ongoing strategy to enhance student enrollment, the State University of Zanzibar (SUZA) recently conducted an extensive outreach campaign across mainland Tanzania.

Led by the SUZA Public Relations Unit in collaboration with the Directorate of Undergraduate Studies (DUS), the initiative aimed to provide secondary school students with critical information about SUZA's admission requirements, academic programs, and higher education opportunities.

Through these engagements, the university sought to inspire and equip students with the knowledge necessary to make informed academic decisions.

Mrs. Khadija Sadiq Mahumba, Head of the Public Relations Unit at SUZA, noted that the school visits took place from February 24 to February 28, 2025, covering multiple regions.

These included Mtwara where schools within the municipality were visited along with Lindi, Morogoro, and Singida. In total, seventy-six (76) secondary schools were privileged to receive guidance from SUZA admission officials.

According to Mrs. Mahumba, the visits had several key objectives: informing students about SUZA's admission criteria and available academic programs, explaining the application process and deadlines, offering insights into university life, and sharing details on sponsorship opportunities and career prospects.

Students from the visited schools actively participated, asking questions about course options, tuition fees, scholarships, and campus life. Many sought clarifications on admission requirements and selection criteria. SUZA officers responded thoroughly, ensuring students understood the necessary steps to apply.

At several schools, students expressed strong interest in joining SUZA but lacked sufficient knowledge about the admission criteria. Financial concerns and inquiries about scholarship opportunities were also prevalent. SUZA officials reassured students by providing detailed explanations and highlighting the role of the Higher Education Students' Loans Board (HES-LB) as a key financial aid resource for eligible applicants.

To further enhance understanding, SUZA distributed informational brochures containing comprehensive guidelines on university

entry and student life. Officials encouraged students to strive for academic excellence and set ambitious educational goals.

Teachers from the visited schools echoed the importance of such engagements, requesting SUZA to continue regular visits that provide students with valuable guidance on higher education opportunities.

Over the years, SUZA has increasingly attracted students from mainland Tanzania, thanks to its proactive outreach efforts. Before the commencement of the current academic year, similar visits were conducted in Arusha, Mwanza, and Tabora, contributing to a rise in student enrollment.

Looking ahead, SUZA plans to extend these visits to all secondary schools in Unguja and Pemba, continuing its commitment to expanding access to higher education.

The impact of these efforts has been evident, with new student enrollments increasing by 8% in the 2023/2024 academic year.

By maintaining these initiatives, SUZA remains dedicated to broadening educational access and fostering academic excellence among prospective students across Tanzania.



## **Whitworth University strengthens partnership with SUZA through Student programs**

**By Our Reporter, SUZA**

The Head of the Kiswahili for Foreigners Department of the State University of Zanzibar, Ms. Shani Suleiman Khalfan, expressed her gratitude to Whitworth University, USA, for consistently choosing SUZA to host its students for Kiswahili language education.

She mentioned that this service has been provided for ten uninterrupted years and hopes that the collaboration will continue to promote the growth of the Kiswahili language.

Speaking at the graduation ceremony, where certificates were awarded and students bid farewell, held at SUZA's Vuga Campus, Ms. Shani thanked the host families for warmly accommodating the visitors.

"Thank you so much for trusting us. I believe this support is not limited to the teachers alone but also extends to the parents. We truly appreciate their help in hosting our visitors so well," she said.

Prof. Megan Hershey, a Political Science in-charge specializing in African Studies from Whitworth University, USA, expressed her satisfaction with SUZA's management for enabling students

to study Kiswahili in conducive classroom environments and welcoming host families.

While giving her gratitude, Prof. Megan mentioned that Kiswahili teaching programmes have been well-coordinated for a long time, promising that the collaboration will continue to promote Kiswahili language development.

She added that the host families significantly contributed to the students' progress, including teaching them other aspects of Kiswahili culture.

During the graduation event, students showcased small performances, such as skits, before the guests. They ex-

pressed their joy in learning and living with host families. "We are happy to have gained great experience in the language.

We think our Kiswahili has significantly improved. For instance, now we can read books, we are putting in individual efforts, and we expect to achieve even more," said one student.

The 15 students who completed their one-month studies also had the opportunity to visit various historical sites, including Jozani Forest Reserve, Jambiani, Kizimbani, Maruhubi, Kijichi, and Nungwi, where they learned about the practical use of Kiswahili in its natural context.

### **Newsletter Editorial Committee**

<b>Chairperson</b>	<b>Mr. Hassan Simba Hassan</b>
<b>Coordinator</b>	<b>Ms. Khadija Sadiq Mahumba</b>
<b>Articles Editor</b>	<b>Dr. Masoud Nassor Mohammed</b>
<b>News Editor</b>	<b>Dr. Rashid Maalim Khamis</b>
<b>News Producer</b>	<b>Ms. Nasima Haji Chum</b>
<b>Photographer</b>	<b>Mr. Hamza Makame Ussi</b>
<b>Newsletter Graphic Designer</b>	<b>Mr. Zedi Abdalla Khamis</b>



## Dr. Mwinyi calls for Youth preparedness for the job market

By Our Reporter, SUZA

The President of Zanzibar and Chairman of the Revolutionary Council, Hon. Dr. Hussein Mwinyi, has called for a feasibility study of vocational training programmes to prepare graduates for the job market and industrial needs.

Hon. President Mwinyi made these remarks in a speech read on his behalf by the Second Vice President of Zanzibar, Hon. Hemedi Suleiman Abdullah, while addressing education stakeholders.

He outlined key recommendations, including fostering collaboration between educational institutions and the private sector to produce graduates with market-relevant skills. Another recommendation was addressing challenges faced by youth, particularly women and special groups, in accessing technical and vocational education and training (TVET), and proposing solutions to these issues.

He also emphasized the need to improve educational curricula and vocational training programmes to meet the rapidly evolving job market demands and to conduct research on the use of Information and Communication Technology (ICT) and innovative technologies.

"It is my hope that research in these areas will enable the government and education stakeholders to make sound decisions that will enhance the vocational training sector and equip Tanzania's youth with modern skills to contribute to national development," said Dr. Mwinyi.

Earlier, SUZA Vice Chancellor, Prof. Moh'd Makame Haji, stated that SUZA is leading in conducting research related to the environment, health, education, and the

economy, which has significantly contributed to improving education policies and development in Zanzibar and Tanzania at large.

He added that conferences like this provide an opportunity for researchers, scholars, and policymakers to exchange knowledge and strengthen the direction of educational research.

Speaking on behalf of the conference organizing committee, Ms. Hannah Simon highlighted that the Tanzania Education Research 2025 initiative is the outcome of extensive work by the organizing committee, led by SUZA, the University of Dar es Salaam through CoICT (UDSM-CICT), the Ministry of Education, Science, and Technology, and the Tanzania

Institute of Education (TIE), in collaboration with FCDO, Canada, British Council, EdTech Hub, and Aga Khan Foundation.

Additionally, the conference focused on key topics such as students dropping out of school, those who remain and return to school, teacher preparation, climate and environmental education, and TVET education and employability.

This fourth conference, hosted for the first time in Zanzibar, involved various education stakeholders from within and outside Tanzania and was sponsored by international and community organizations as well as the Government of the United Republic of Tanzania.

## SUZA leads the way in the digital economy

By Our Reporter, SUZA

The Vice Chancellor of the State University of Zanzibar (SUZA), Prof. Moh'd Makame Haji, has encouraged the university to seize the opportunity of collaborating with visitors from technologically advanced countries, which aligns with national policies aimed at strengthening the digital economy.

He made these remarks on January 10, 2025, at SUZA's headquarters during a three-day training session for guests from Jordan, Morocco, and Lebanon on assisting science students in utilizing modern technology.

He explained that through this collaboration, SUZA will produce more experts in this field, who will achieve significant milestones in high-performance computing by gaining broader insights into global advancements.

Dr. Maryam Masoud Khamis, a lecturer in SUZA's Department of Computer Science, noted that the project, funded by the European Union, aims to assist science students in regions lacking such technology to access and utilize it effectively.

Students will be able to use the technology even in areas without network coverage, which will address equipment shortages and enable them to access technology at any time, even at night.

"This is an important opportunity as it will help address equipment shortages and ensure availability for students at any time," she stated.

She added that SUZA is developing a Cybersecurity curriculum for undergraduate and master's students, emphasizing that this is significant since SUZA is the first to introduce such a programme.

She explained that SUZA has advanced in this area as it offers cybersecurity courses for undergraduate students.

The training session involved more than 20 guests, and on the final day of the visit, additional students who had previously missed out were also able to participate.

Speaking on the participation of women in technology, she expressed pride in being one of them but noted the poor involvement of women in this field. She advised making good use of this laboratory, as it will also be accessible to non-SUZA students.



## SUZA prepares skilled leaders

By Our Reporter, SUZA

The Deputy Minister of Community Development, Gender, Elderly, Women, and Children, Hon. Anna Athanas Paul, stated that the State University of Zanzibar (SUZA) is preparing skilled leaders capable of managing the nation's future plans and strategies.

While delivering her speech at the Student Welfare Day celebrations organized by the SUZA Students' Organization (SUZASO) held at the SUZA Tourism Institute in Maruhubi Campus, Hon. Anna expressed satisfaction with the execution of SUZASO's responsibilities, showcasing the maturity and excellence of its leadership.

Among the initiatives that impressed her was the creation of the Ministry of Student Welfare, allowing welfare-related activities to be handled by students rather than the Ministry responsible for people with disabilities.

"This is a great innovation, and it reflects visionary maturity. It is clear evidence that SUZA is indeed preparing excellent and skilled leaders through SUZASO," she said.

Speaking on the issue of harassment, she noted that the government's mission to produce highly skilled youth will not be realized

if acts of harassment, particularly against women and children, persist, undermining the goals of delivering quality education. She urged students not to remain silent in the face of harassment incidents and to report them to legally established authorities.

She also highlighted that the Revolutionary Government of Zanzibar, under the leadership of President Dr. Hussein Mwinyi, has made significant efforts in infrastructure development, including modern schools, higher education improvements, and constructing new SUZA buildings.

Earlier, SUZA Vice Chancellor Prof. Moh'd Makame Haji stated that SUZA is highly relevant to Student Welfare Day by offering quality education through its 60 programs spanning Certificate, Diploma, Bachelor's, Master's, and Doctoral levels.

"All programs are delivered at a high standard to enable graduates to utilize their knowledge to drive change and contribute to national development," emphasized Prof. Haji.

On combating harassment, Prof. Haji noted that the university has established Gender Desks in all its campuses, represented by both teachers and students, to handle complaints.

"The university also provides ed-

ucation to 58 special needs students, including those with visual impairments, mobility challenges, and speech difficulties. They are excelling thanks to well-planned education strategies," Prof. Haji highlighted. Prof. Haji also mentioned other student welfare achievements, including a dedicated budget for the Student Government, student inclusion in key SUZA decision-making meetings, participation in national and international sports events, the provision of entrepreneurship centers, addressing modern technological needs, and establishing a special business incubation hub for students.

The SUZA Student Government President, Mwanamkuu Jega Bakari, expressed gratitude to the SUZA administration for their support in both academics and student government activities.

During the event, the Student President requested the Ministry of Community Development, Gender, Elderly, Women, and Children to collaborate with the university in providing training on social welfare issues, a proposal the guest of honor accepted.

The SUZA Students' Organization Minister for Welfare, Khatib Nassor, noted that the existence of the government has fostered unity and collaboration between SUZA's teachers and students.



## Education Research Conference 2025 concludes

By Our Reporter, SUZA

The two-day Education Research Conference 2025, organized by the State University of Zanzibar (SUZA) in collaboration with the University of Dar es Salaam (UDSM), officially concluded on February 26, 2025.

Closing the conference at the SUZA Maruhubi Campus hall, the Zanzibar Deputy Principal Secretary for Academics in the Ministry of Education and Vocational Training, Dr. Mwanakhamis Adam Ameir, emphasized that the discussions held during the Education Research Conference would yield positive outcomes if implemented practically to address the challenges facing the education sector.

She noted that she believes all the topics had experienced contributors from the education sector, and that they could bring about significant changes to education and achieve the intended goals.

"The insights shared during this conference are meant to be implemented practically to overcome existing challenges and achieve the desired objectives," she said.

During the conference, four topics were discussed, including teacher preparation, curriculum and environment, the issue of school dropouts, and research and innovation.

These topics were thoroughly analyzed to address progress and challenges in the sector.

Speaking at the event, Tanzania's Commissioner of Education, Prof. Lyambwene Mtahabwa, expressed gratitude to all education stakeholders from within and outside Tanzania for successfully completing the conference.

The State University of Zanzibar (SUZA) collaborated with the University of Dar es Salaam to host the Education Research Conference 2025, which brought

together more than 500 participants, including scholars, policymakers, and education stakeholders from both within and outside the country.

The aim of the conference was to strengthen the use of ICT in education, promote continuous training programmes for teachers and researchers, and ensure that research findings inform the development of better education policies.

## SUZA Council meets with Academics

By Our Reporter, SUZA

The State University of Zanzibar (SUZA) Council Chairperson, Ms. Hamida Mohammed Ahmed stated that the Council's role in implementing its duties has contributed to creating a conducive environment for the university's service delivery.

Speaking during a joint meeting with academics and members of various SUZA committees held at SUZA's headquarters in Tunguu, South Unguja, on January 28, 2025, she noted that SUZA has experienced significant changes in the provision of education and the improvement of its infrastructure.

She also expressed gratitude to the Council members and academics for their strong collaboration, which contributes to achieving the set goals, and promised that such meetings would continue regularly to address emerging challenges.

Earlier, the SUZA Vice Chancellor, Prof. Moh'd Makame Haji, explained that SUZA collaborates with various stakeholders, including experts

from the Tanzania Commission for Universities (TCU) and institutions with high qualifications and experience in service delivery.

"We are creating a friendly environment to take the university to the next level of success. It should be understood that some activities carried out by SUZA must pass through the central government before implementation," he reminded. He added that despite the significant achievements made, there is a need to place great emphasis on research.

The Chairperson of SUZA's Students' Welfare Committee, Ms. Salma Saadat, proposed that students should be encouraged to present their challenges to the Students' Welfare Committee.

The President of the State University of Zanzibar Students' Organization (Suzaso), Mwanamkuu Jega, advised academics to use polite language with students when giving instructions. She confirmed their readiness to be guided by academics, as they are the first witnesses of the progress in their education development.



## Community urged to encourage Youth in Education

By Our Reporter, SUZA

The State University of Zanzibar Students Organization (SUZASO) has organized a visit to Kidoti Ward (Shehia), located in North 'A' District in North region - Unguja with the aim of offering charity to the villagers of that Shehia and promoting the importance of education in overall development.

The students' dedication demonstrates the power of youth in bringing positive change. During the visit, the Vice Chancellor of SUZA, Prof. Moh'd Makame Haji, accompanied the students and urged the community to encourage young people to seize educational opportunities from the lower levels in order to create a foundation for pursuing higher education.

The Vice Chancellor of State University of Zanzibar (SUZA), Prof. Moh'd Makame Haji, has called on the community to motivate young people to seize educational opportunities from lower levels in order to create a foundation for higher education.

Prof. Haji made this appeal while speaking to villagers of this Shehia alongside the leadership of the State University of Zanzibar Students' Organization (SUZASO). The visit was part of an initiative to provide charity to people with special needs during the holy month of Ramadhan.

